## TOT ni bandika bandua Tamasha la Dk. Samia



Uk. 21

## Mkenya anayemiliki hospitali nchini Marekani



Uk. 15

## Zijue faida za ukwaju kwa afya ya binadamu



Uk. 14

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo




| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00060 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Aprili 17 - 23, 2024 |

## Mikoa 5 kuunganishwa umeme Gridi ya Taifa

Uk. 2



## Mufti Mkuu awamwagia pongezi Samia, Mwinyi

Uk. 3



## Timu Nchimbi kila la kheri, mmeanza vizuri

Uk. 12



# UWT yamwahidi mazito Dk. Samia



Wamepita viongozi wengi, lakini kwa uthubutu huu wa Mama (Samia), tunamuunga mkono kwa asilimia 100...

Uk. 4

## Kinana: Chagua viongozi kwa uwezo, si kabila, dini



Mtu mmoja kwenye kabila lako akipata cheo anakusaidia nini hasa wewe mwenyewe? Uko kijijini kule, mngekuwa mnagawana mshahara sawa

# Mikoa 5 kuunganishwa umeme Gridi ya Taifa

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amejipatia wizara yake fedha nyingi kwa ajili ya kuondoa kero ya umeme nchini na kwamba mikoa mitano Kigoma, Katavi, Rukwa, Lindi na Mtwara, itaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua Wiki ya Maonesho ya Nishati yanayofanyika katika viunga vya Bunge jijini Dodoma.

"Rais Samia aliagiza tuhakikishe wananchi wanapata umeme wa uhakika, tuache stori kwa kuwa wakikosa huduma hiyo, wanalalamika na Mama yetu hataki kusikia malalamiko ya wananchi wake," alisema.

Alisema maonyesho hayo si kwa ajili ya kupiga picha, bali ni ya kuwasikiliza wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi ili wakirudi majimboni, wakawaeleweshe vizuri changamoto na juhudi za serikali katika kutatua kero zao.

"Siku ya Pasaka, nilisahau kabisa kufufuka kwa Yesu, nawapongeza sana Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kazi kubwa waliyoifanya siku ile. Hawa wafanyakazi wa Tanesco kwa kweli wanafanya kazi sana hitilafu ya Pasaka ilikuwa ifanyiwe kazi na kukamilika kwa muda wa siku nne, lakini walifanya kazi kwa saa tisa na umeme ukarejea nchi nzima, nawapongeza sana," alisema na kuongeza:

"Mkurugenzi Mkuu wa Tanesco, unapowasikiliza wabunge hapa kama jambo haliwezekani wajibu ukweli usiwadanganye, eti tunalichukua, hapana wapeni majibu ya uhakika na yale yanayowezekana."

Alisema baada ya maonyesho hayo, wataandaa taarifa ya kila lalamiko na jinsi lilivyosikilizwa ili kuliwasilisha kwa Waziri Mkuu.

"Lazima tufanye kazi, Tanesco bado kuna mahitaji makubwa ya umeme na tunajiandaa kuuza kwa majirani zetu," alisema.

Alisisitiza kwamba baada ya Rais kufungua nchi, Mkoa Pwani una viwanda zaidi ya 30 na vinahitaji umeme mwingi, hivyo, serikali inahakikisha mahitaji hayo yanakamilika.

Alisema ndoto ya kuuza umeme kwa majirani kama Uganda, Kenya na Zambia, sasa wakati wake umefika.

Kwa upande wa Zanzibar alisema tayari maboresho yanafanyika kuongeza nguvu kubwa kutoka Tanga kwenda Pemba na kutoka Dar es Salaam kwenda Unguja kwa hiyo wizara hiyo inapaswa kusimama katika kutenda kuliko kusema maneno.

Aidha, aliwataka wabunge kutoa maoni na ushauri katika maonyesho hayo ikiwamo mahali ambapo hawafanyi vizuri ili baada ya maonesho wapate semina ya kufafanua yale ambayo yatahitaji majibu na ufafanuzi.

"Nawatangazia Watanzania, wabunge ni watu wa kwanza kufuatilia watu wanaowawakilisha kama wanapata umeme si kwa kusema bungeni bali hata kwa kwenda ofisi za wizara na shirika hiyo, alisema na kuongeza:

"Nawatolea na siri, katika vikao vyetu vya Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ni wakali sana walishaniweka kitimoto wakidai wanataka umeme hawataki stori, kwa hiyo tuwasikilize na tukayafanyie kazi yale yatakayoboresha upatikanaji wa umeme, kama sasa hakuna tena mgawo," alisema.

Akizungumzia kuhusu kuunga mkono ajenda ya Rais Samia ya matumizi ya nishati safi na salama, alisema mara ya mwisho kibali cha kuchimba gesi kilitolewa mwaka 2006, lakini wameshapata kibali kingine cha leseni ya kuanza kuchimba na wataanza kuchimba.

Aidha, alisema anataka wakazi wa Mkoa wa Mtwara waone umuhimu wa kutumia gesi majumbani na nyingine watauza nchi jirani.



Aibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko

# Mufti Mkuu awamwagia pongezi Samia, Mwinyi

Na Mwandishi Wetu

MUFTI Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, amewapongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa uzalendo uliotukuka wa kutunza na kuzilinda Tunu za Muungano kama zilivyoasisiwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Alitoa pongezi hizo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kabla ya kufanyika dua ya pamoja ya kuombea nchi.

Alisema Baraza limepokea mwaliko wa kushiriki dua hiyo itakayofanyika Dodoma na kuongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, hivyo, anatoa wito kwa Waislamu wote kushiriki katika dua hiyo.



Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi

"Napenda kuchukua fursa hii kuwaalika viongozi na waumini wote wa Kiislamu waliopo mkoani Dodoma na wilaya zake na mikoa jirani, kujitokeza kwa wingi kushiriki dua hiyo itakayofanyika Aprili 22, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri," alisema.

Alisema kama Waislamu wa Tanzania wana kila sababu ya kujivunia mafanikio ya miaka 60 ya Muungano kwani katika kipindi chote, nchi ina utulivu, amani, umoja na mshikamano.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Tumeshikamana na Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa letu.'





Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua kwa helikopta athari zilizosababishwa na mafuriko yaliyotokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini katika maeneo ya Taweta, Masagati, Utengule na Malinyi jana. (Picha: Ofisi ya Waziri Mkuu)

# Kasi ya wizi wa misalaba makaburini watisha Mbinga

Na Claudia Kayombo, Mbinga

BAADHI ya wafanyabiashara wa vyuma chakavu, wameanza kuvamia makaburi na kung'oa misalaba ya chuma wilayani Mbinga na kuiuza kama chuma chakavu.

Akizungumzia wizi huo, Padri Witney Ngahi, alikemea tabia hiyo akisema inavuka mipaka hadi kuwaibia marehemu misalaba makaburini.

Padri Ngahi ambaye ni Paroko wa Parokia ya Mbinga, alionesha masikitiko hayo hivi karibuni wakati wa Misa Takatifu parokiani hapo.

Kemeo la Padri Ngwahi limekuja siku chache tangu kusambaa mitandaoni picha ya mtu wilayani hapa aliyekutwa na misalaba ya chuma akilenga kwenda kuiuza kama vyuma chakavu.

Alisema zaidi ya misalaba 25 ya vyuma imeibiwa kwa kung'olewa katika makaburi ya parokia.

Padri Ngwahi alisema wezi wa misalaba wanapaswa kutambua kuwa kabla misalaba hiyo kusimikwa makaburini, kiongozi wa dini huibariki na hivyo kuwa visakramenti.

> Kemeo la Padri Ngwahi limekuja siku chache tangu kusambaa mitandaoni picha ya mtu wilayani hapa aliyekutwa na misalaba ya chuma akilenga kwenda kuiuza kama vyuma chakavu.



# Dk. Nchimbi atoa rai viongozi na wazee kuwalinda watoto, vijana

**Na Mwandishi Wetu, Sumbawanga**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ametoa wito kwa

viongozi wa serikali, taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali, wazee na viongozi wa dini, kwa pamoja kuwa sehemu ya kuendelea kuwa walinzi wazuri kwa watoto na vijana.

Balozi Dk. Nchimbi ametoa rai hiyo kutokana na kusikitishwa na mmomonyoko wa maadili uliyokithiri nchini.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza kwenye mkutano uliokutanisha Mabalozi wa Mashina wa CCM, viongozi wa serikali, taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali, wazee na viongozi wa dini mjini Sumbawanga mkoani Rukwa juzi.

Aidha, Balozi Dk. Nchimbi amekemea vikali tabia hiyo kwa baadhi ya wazazi na walezi wanoshindwa kutimiza wajibu wao vizuri na kusababisha watoto na vijana wengi kuwa na tabia zisizofaa katika jamii.

Aidha, amewashukuru viongozi wa dini kwa kuendelea kuliombea Taifa kuwa na amani na utulivu wakati wote.

"Viongozi wa dini mnafanya kazi kubwa sana katika kuiombea na kuilinda amani na mshikamano wa nchi yetu, alisema na kuongeza:

"Kuna wakati mnasali na kutufanya hadi anayesikiliza maombi, kujiona na kutuambia kwamba unayo sababu ya kuilinda amani ya nchi yetu. "

Alisema: "Nawaomba viongozi wa dini, endeleeni kutoa maombi ya kuliombea Taifa katika masuala ya mmomonyoko wa maadili, kumekuwa na mmomonyoko makubwa ya maadili kwa vijana na watoto."



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akimsikiliza mmoja wa wananchi waliojitokeza kumlaki msafara wake ulipowasili katika Soko la Mazao katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe jana kuangalia maendeleo ya maboresho ya soko hilo na kusikiliza kero za wafanyabiashara. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo.

# Wanasheria wafundwa utamaduni wa kujisomea

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

JAJI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Ibrahim Hamis Juma, amewataka wanafunzi wanaohitimu masomo ya sheria kuwa na utamaduni wa kujisomea kwa kuwa dunia sasa hivi inapitia mabadiliko makubwa ya matumizi ya teknolojia kwenye utendaji wa kazi.

Aliyasema hayo jijini hapa juzi wakati akiongoza maadhimisho ya Siku ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) ambayo yameongozwa na kaulimbiu, "Uimarishwaji wa kliniki za sheria vyuo vikuu katika kukuza na kupanua wigo wa upatikanaji wa haki Tanzania."

"Maarifa katika Karne ya 21, huletewi, unatafuta na unatafuta kwa kusoma, bahati nzuri tuna mifumo mizuri ya teknolojia ambayo inatuwezesha kusoma na Mwalimu Nyerere alisema wenzetu wanapotembea, sisi tunapaswa kukimbia," alisema.

Alisema katika zama hizi za teknolojia, wanapaswa kukimbia ili kwenda sawa na wenzao kwani kasi ya mabadiliko ni kubwa.

Aidha, alisema kwa sasa kuna changamoto kubwa ya mrundikano wa mawakili katika maeneo ya mjini, hivyo amewaomba wanafunzi hao pindi watakapohitimu masomo yao, kusambaa katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo vijijini ili kuwasaidia wananchi wanaopitia changamoto za kisheria.

"Mnapokutana na wananchi katika kutoa msaada wa kisheria, moja ya majukumu yenu ni kuhakikisha mnafahamu changamoto za kisheria zinazowakabili wananchi wa kawaida, kuna watu wapo Tanzania, lakini hawajui uhalisia wa changamoto zinazowakabili wananchi wa kawaida," alisema.

Pia alisema hakuna uwekezaji mkubwa kama uwekezaji wa maarifa kwani Karne hii ya 21 inahitaji zaidi maarifa ili kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo cha Udom, Profesa Lughano Kusiluka, ameiomba Mahakama kuwa na matawi ya vyuo vya sheria kila kanda ili kuwasaidia wanafunzi wanaotaka kusoma sheria kubakia katika maeneo yao kuliko kusafiri kufuata vyuo hivyo sehemu za mbali.

"Mimi nashauri, ila mtaangalia kama litakuwa ni jambo jema kwa kuwa tuna majaji wengi kwenye kanda na hao ndiyo wa kuwafundisha hawa kwenye mafunzo kwa vitendo, kwa kuwa tuna Tehama ambayo inaweza ikawasaidia watu kusoma na vitendo, nadhani ingekuwa ni vizuri Mahakama ikafikiria kuwa na matawi ya Shule za Sheria angalau katika kila kanda ili vijana hawa wasome huko," alisema.

Alisema wamekuwa wakishirikiana vyema na Wizara ya Katiba na Sheria na wadau wengine kama njia ya kuwajengea uwezo na ufanisi mkubwa vijana wanaohitimu masomo yao ya sheria.

Maadhimisho ya Siku ya Sheria Udom mwaka huu yanaadhimishwa kwa mara ya tatu tangu yaasisiwe.



Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Ibrahim Hamis Juma

# RC awatwisha zigo madaktari wafawidhi

**Na Claudia Kayombo, Songea**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Ahmed Abbas Ahmed, amewataka madaktari wafawidhi wa vituo vya afya na madaktari wakuu wa wilaya, kusimamia ukusanyaji wa mapato katika vituo vya kutolea huduma za afya.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Ahmed Abbas Ahmed

Aliyasema hayo wakati akifungua Mkutano wa Mwaka wa Wadau wa Bohari ya Dawa (MSD), Kanda ya Iringa, uliofanyika mjini Songea ambao ulihudhuriwa na waganga wakuu na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Ruvuma pamoja na wataalam wa maabara.

Alisema hatua ya kusimamia ukusanyaji wa mapato katika vituo vya kutolea huduma za afya, itaviwezesha kulipa madeni inayodaiwa na MSD baada ya kupokea shehena ya bidhaa ili kuepusha madeni yasiyo ya lazima.

Alisema hatua ya kuvisimamia vituo vya kutolea huduma za afya, itawezesha kununua bidhaa za afya na kusimamia mnyororo wa ugavi wa bidhaa hizo.

Aidha, aliwataka kushirikiana ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi hasa wagonjwa wanaofika hospitali kupata matibabu.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kuongeza na kutenga fedha kwa ajili ya kununua bidhaa za afya ili kuboresha huduma hizo na kwamba kila mmoja ana wajibu wa kusimamia matumizi ya vifaa hivyo ili kuleta tija kwa wananchi.

Alisema ikiwa watatekeleza hayo, wananchi watapata huduma bora za afya katika maeneo yao bila kuwapo kwa manung'uniko na kujenga imani kwa wananchi dhidi ya serikali yao.

# UWT yamwahidi mazito Dk. Samia

**Na Allan Vicent, Tabora**

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) mkoani Tabora, umeahidi kumuunga mkono kwa asilimia 100 Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa utendaji wake wa kazi, huku ukisema watazunguka mkoa mzima kuyasemea mazuri yake, kuhamasisha wanawake kumuunga mkono na kumpigia kura za ndiyo.

Katibu wa UWT Mkoa wa Tabora, Rhoda Madaha, alisema kuwa miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani, imeleta neema kwa wananchi katika sekta zote ikiwemo elimu, afya, maji, nishati na miundombinu ya barabara.

"Wamepita viongozi wengi, lakini kwa uthubutu huu wa Mama (Samia), tunamuunga mkono kwa asilimia 100, tutazunguka mkoa mzima kuyasema mazuri yote aliyoyafanya na tutahamasisha wanawake wote wamuunge mkono," alisisitiza.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na gazeti hili la UELEKEO juzi, lililotaka kujua mikakati ya UWT kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani hapo mwakani.

Alisema kasi, weledi na ubunifu wa Rais Dk. Samia, vimewezesha miradi mikubwa ya kimkakati kama ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), Bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Tanga, kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kutoa fursa za ajira kwa wananchi wengi.

Alitaja mradi mwingine kuwa ni Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere ambalo tayari limeanza kuongeza nguvu ya umeme nchini baada ya kinu cha kwanza kuwashwa, matokeo chanya yameanza kuonekana na mgawo wa umeme sasa umeisha.

Alisema Rais Dk. Samia ametekeleza miradi mingi ya maji mikoa yote nchini na mingine inaendelea kutekelezwa kama Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria na Mradi wa Maji wa Miji 28, ambayo imewafuta machozi wanawake.

Alisema wanawake walikuwa wakihangaika kufuata maji umbali mrefu, lakini Mama (Dk. Samia), amemaliza kero hiyo, sasa maji yameendelea kusogezwa karibu zaidi na wananchi ili kumtua mama ndoo kichwani.

Naye Mwenyekiti wa UWT Mkoa, Mwanne Mchemba, alisema Rais Samia amefanya mambo makubwa, hawawezi kukaa kimya, hivyo aliahidi kuwa mwakani watatembea nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, kitongoji kwa kitongoji, kijiji kwa kijiji, kata kwa kata na tarafa kwa tarafa ili kumwombea kura.

Alieleza kuwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, nchi ipo katika mikono salama, wanawake wanajivunia kuwa na kiongozi mwanamke, mchapakazi mahiri na wa viwango, hivyo wakaahidi kumuunga mkono na kumpa kura za kishindo.

Aidha, aliwataka wanawake wote mkoani Tabora, kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na ule wa mwakani ili kuwapigia kura wagombea wote wa CCM huku akiwaomba wote wenye sifa na uwezo kujitokeza kugombea pia.



**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akimpa pole na kumfariji Mwanakheri Mussa Yussuf, mjane wa marehemu Mzee Mussa Abdulrahman ambaye alikuwa rafiki wa familia na jirani wa karibu. Alifariki dunia usiku wa kuamkia jana Mtaa wa Mombasa, Zanzibar ambapo Rais Dk. Samia alifika kutoa pole msibani Kwahani Mchangamwingi, Zanzibar jana.**

# Kinana: Chagua viongozi kwa uwezo, si kabila, dini

> **Sasa usimpe mtu nafasi ya uongozi kwa sababu ya kabila lake, dini au umbile, usimhukumu, hayo ni mambo ya kizamani sana.**



**Na Mwandishi Wetu, Rorya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, amewataka wanachama wa chama hicho na wananchi kwa ujumla, kuacha tabia za ukabila na udini akieleza kuwa ni mambo ya kizamani na yanawagawa.

Akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Kinana alisema nchi kuwa na makabila, ni jambo la kawaida, ila ukabila ni jambo baya.

Alisema hayo baada ya baadhi ya wajumbe kuibua hoja kwamba kuna mambo yanafanyika katika Wilaya ya Rorya ambayo yanaashiria kuwepo kwa changamoto ya ukabila miongoni mwao.

Alisema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ametoka mkoa huo na ni kabila dogo sana na aliongoza nchi kwa miaka 24, na kwamba alipendwa, aliheshimiwa, alithaminiwa na alitukuzwa siyo kwa sababu ya ukabila bali kazi aliyokuwa anaifanya, utendaji na uadilifu wake uliomfanya aheshimike Tanzania, Afrika na duniani.

"Sasa usimpe mtu nafasi ya uongozi kwa sababu ya kabila lake, dini au umbile, usimhukumu, hayo ni mambo ya kizamani sana, tuangalie mtu ana uwezo atafanya kazi, atajituma na kujitolea, mnampima kwa vigezo siyo kwamba huyu ni ndugu yangu," alisema na kuongeza:

"Mtu mmoja kwenye kabila lako akipata cheo anakusaidia nini hasa wewe mwenyewe? Uko kijijini kule, mngekuwa mnagawana mshahara sawa, kila mmoja anakuletea Sh. 300,000 kutoka kwenye mshahara wake kwa sababu ni kabila lako sawa... wekeni watu kwa uwezo."

Aidha, alieleza kuwa jambo ambalo Baba wa Taifa aliwaachia kuwa ni umoja wa kitaifa, akitolea mfano kwamba kuna nchi jirani, (hakuzibainisha kwa majina), kwamba mtu hawezi kuwa gavana wa jimbo kama anatoka sehemu nyingine, lakini Tanzania wanafanya kazi nchi nzima.

# TBS yatoa leseni 2,106 kwa wazalishaji bidhaa

> **TBS iliendesha mafunzo kwa wadau 5,789 kutoka mikoa mbalimbali nchini na kwamba shirika hilo linaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo (MSEs) na wazalishaji ili kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama na hatimaye kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.**



**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetoa jumla ya leseni za ubora wa bidhaa 2,106 kwa wazalishaji mbalimbali wa bidhaa hapa nchini sawa na asilimia 105.3 ya lengo la kutoa leseni 2,000 katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kati ya leseni hizo, 1,051 zilitolewa bure na kwa wajasiriamali wadogo.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athumani Ngenyu alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utendaji na mafanikio ya taasisi hiyo kwa wahariri na waandishi wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam chini ya uratibu wa Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu.

Dk. Ngenyu alisema mbali ya kutoa leseni hizo, pia TBS iliendesha mafunzo kwa wadau 5,789 kutoka mikoa mbalimbali nchini na kwamba shirika hilo linaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo (MSEs) na wazalishaji ili kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama na hatimaye kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Aidha, Dk. Ngenyu alisema TBS imewekeza kwenye ununuzi wa vifaa vya maabara vya kisasa (state-of-the-art-equipment) kwa kutumia fedha za ndani pamoja na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, jumla ya viwango 1,721 vya kitaifa, viliandaliwa sawa na asilimia 101.2 ya lengo la kuandaa viwango 1,700 na kwamba viwango hivyo viliandaliwa katika nyanja mbalimbali.

Aidha, alisema TBS imeshiriki katika uandaaji wa viwango vya kibiashara vya Afrika Mashariki na Afrika.

Vilevile, alisema Shirika linatarajia kuanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Kanda ya Ziwa (Mwanza)

Inayotarajiwa kuhudumia mikoa sita ya Mwanza, Kagera, Mara, Geita, Shinyanga na Simiyu.

Kadhalika, alisema TBS inakusudia kujenga maabara Kanda ya Kaskazini Arushaitakayohudumia mikoa minne ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

Alisema kwa sasa TBS ina maabara 12 zilizopo Ubungo jijini Dar es Salaam ambazo zimehakikiwa na kupatiwa cheti cha ithibati ya umahiri wa kimataifa (accreditation) na hivyo kuwezesha majibu ya sampuli kutoka katika maabara hizo kuaminika kokote duniani na hivyo kurahisisha biashara.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

## Stendi hii itaanza kazi lini?

Kumekuwa na adha kubwa ya mahala pa daladala kushushia abiria katika eneo la Gerezani (wengine wanaita Shule ya Uhuru au Kariakoo) Dar es Salaam, hususani kwa zinazotokea Temeke.

Hii ni kwa sababu stendi ya daladala hizo bado inatengenezwa na hivyo daladala zinashushia abiria kwenye Barabara ya Shaurimoyo. Lakini barabara hiyo kwa sasa imejaa maji na hivyo abiria wanalazimika kushushiwa mbali au kwenye tope.

Tunajiuliza, kwa nini stendi hii muhimu imechukua muda mrefu kukamilika? Je, kwa nini hii barabara ya Shaurimoyo, hususani katika eneo hili la Shule ya Uhuru haiboreshwi?




## MAONI YA MHARIRI

# Tujitenge mbali na ukabila kwenye chaguzi

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, amewataka wanachama wa chama hicho na wananchi kwa ujumla, kujitenga na tabia za ukabila na udini akieleza kuwa ni mambo ya kizamani na yanayowagawa wananchi.

Kinana ameyasema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Rorya mkoani Mara ambako amefanya ziara. Amesema nchi kuwa na makabila, ni jambo la kawaida, ila ukabila ni jambo baya na la kukemewa mithili ya pepo mchafu.

Makamu Mwenyekiti huyo amesema hayo baada ya baadhi ya wajumbe kuibua hoja kwamba kuna mambo yanafanyika katika Wilaya ya Rorya ambayo yanaashiria kuwepo kwa changamoto ya ukabila miongoni mwao. Sehemu kubwa ya wenyeji wa Rorya ani Wajaluo lakini pia kuna Wakurya na Wajita wachache.

Kinana amekemea ukabila na udini wakati mwafaka hasa kwa kuzingatia kwamba nchi yetu inaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na mwaka kesho tunaingia kwenye uchaguzi mkuu.

Huwa inasemwa kwamba changamoto kubwa kwa demokarsia barani Afrika sio fahari ya kuwa na makabila mengi, bali ni watu 'wajinga' kutumia makabila hayo kuendeleza siasa za ubinafsi ambazo zinachochea siasa za kikabila. Tusiende huko.

Ndio maana Kinana amewaonya wananchi kutompa mtu nafasi ya uongozi kwa sababu ya kabila lake, dini au umbile lake. Anasema cha kuangalia ni kama mtu anayetaka uongozi ana uwezo na atafanya kazi kwa kujituma na hata kujitolea.

Kinana amesisitiza kwamba mgombea apimwe kwa vigezo hivyo vya uwezo wake ni si kwa sababu ni ndugu yako, dini yako au kabila lako.

Kimsingi, kama alivyosema Kinana, ukabila na udini ni ubaguzi hatari na sumu ya maendeleo. Mambo haya hatuyakemei kwenye chaguzi tu bali wakati wote ubaguzi huu wa ukabila, udini, umajimbo au rangi ya mtu ni wa kuogopwa kama Uviko-19.

Juzijuzi hapa, Rwanda imeadhimisha miaka 30 ya mauaji ya kimbari ambayo karibu watu milioni moja waliuawa na 'kosa' lao kubwa ni kuzaliwa tu katika kabila Kitutsi.

Ubaguzi wa ukabila au dini, umesababisha watu kukosa haki zao, watu kukosa ajira, kukosa elimu na huduma nyingine muhimu lakini na hata kuuawa.

Shime Watanzania, tusilee kabisa ubaguzi wa kikabila na kidini.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |


## JICHO LANGU

# Kila mdau ahamasishe usomaji vitabu

JUMAMOSI ya Aprili 13, 2024, kulikuwa na tukio adhimu la Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi Bunifu. Malengo ya tuzo hiyo, pamoja na mambo mengine ni kuhamasisha uandishi wa vitabu miongoni mwa Watanzania.

Lakini wakati tuzo hiyo ikihamasisha uandishi wa vitabu, kumekuwa na shida ya mwamko mdogo wa usomaji vitabu.

Akizungumza kwenye tuzo hizo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Musa Sima alisema teknolojia pia imechangia uvivu wa kusoma vitabu ambapo watu wanapenda kusoma vitu vifupifupi kwenye mitandao.

Hivi karibuni, muuzaji mmoja wa vitabu katikati ya jiji la Dar es Salaam, alikiririwa na TBC Digital akisema kwamba wateja wake wakubwa ni wazungu na ndio maana ana vitabu vingi vya lugha za kigeni!

Alisema ni nadra kuona wazungu wakipita mara mbili tatu bila kununua kitabu lakini anaweza kumaliza wiki hajauza kitabu hata kimoja kwa Mtanzania hata kama wanaopita pale ni mamia kwa maelfu!

Kinachotakiwa bila shaka kwa sasa ni kila mtu na kila mdau kupenda kusoma na kuhamasisha pia wengine usomaji wa vitabu, magazeti na majarida.

Ndio maana Sima wakati wa Tuzo aliitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kushirikiana na wabunge pamoja na wadau wengine kurejesha hamasa ya usomaji wa vitabu nchini.

Alisema usomaji wa vitabu, mbali na kumpa mtu maarifa unaimarisha lugha na utamaduni.

Hii ilinikumbusha wakati fulani Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilizindua vitabu vinne na Katibu Mkuu wa Baraza hilo wakati huo, Kajubi Mukajanga, alieleza kusikitishwa kwake na hali ya usomaji wa vitabu na magazeti ilivyoshuka kwa kiwango kikubwa nchini.

Alisema kwa kuwa yeye pia ni mchapaji, anakumbuka miaka ya nyuma, walikuwa wanachapa kitabu cha riwaya wastani wa nakala 10,000, lakini mwaka haushi wanalazimika kuchapa nakala nyingine.

"Lakini sasa, licha ya idadi ya Watanzania kuongezeka maradufu (zaidi ya watu milioni 55), mtu anachapisha nakala 1,000 lakini mwaka unaisha hajamaliza kuziuza!" Alisema akionesha masikitiko.

**Lakini sasa, licha ya idadi ya Watanzania kuongezeka maradufu (zaidi ya watu milioni 55), mtu anachapisha nakala 1,000 lakini mwaka unaisha hajamaliza kuziuza!**

Alisema tatizo la kushuka usomaji linachangiwa na walimu ambao badala ya kufundisha watoto kupata maarifa wao wanawafundisha kujibu mitihani hivyo inashusha ari ya kutafuta maarifa kwa kusoma vitabu!

Kwa msingi huo alitoa rai kwa Watanzania wakiwemo walimu kubadilika na kujenga utamaduni wa kusoma kwa sababu maarifa yako kwenye vitabu na machapisho mbalimbali.

Katika kuongeza hamasa ya kusoma, sisi wazazi pia tuna dhima kubwa ya kujenga utamaduni wa kusoma miongoni mwa watoto wetu.

Tutaujenga huu utamaduni kwa sisi wenyewe kubadilika na kupenda kusoma machapisho mbalimbali, kununua vitabu vikiwemo vya riwaya ambavyo mbali na maarifa husaidia sana katika kufundisha lugha na kuhakikisha watoto wetu pia wanavisoma.

Tuwape watoto muda mfupi wa kuangalia televisheni na mrefu wa kusoma na kisha kuwauliza maswali kuona kama wameelewa walichosoma.

# CCM tusibwete, uchaguzi huu unaushindani mkubwa-Kinana

- **Asema sheria ya uchaguzi imetoa nafasi ya ushindani**
- **Ni muhimu kuisoma na kuilewa sheria ya uchaguzi**
- **Akemea ukabila , asisitiza umoja na mshikamano**

**Na Mwandishi Wetu, Rorya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara Abdulrahman Kinana amewaeleza wanachama wa Chama hicho uchaguzi wa Serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani utakuwa na ushindani hivyo wasibwete.

Akizungumza katika kikao kazi cha ndani na Wana CCM Wilaya ya Rorya mkoani Mara ambako anaendelea na ziara ya kikazi, jana, Kinana amesema kuna kanuni za uchaguzi za vyombo vya dola.

"Tunatakiwa tufuate maadili ya uchaguzi na tufanye kila linalowezekana na nimepata ahadi nyingi kwamba tutashinda kwenye uchaguzi unaokuja wa Serikali za mitaa mwaka huu, niwambie utakuwa na ushindani.

"Kwa sababu zile sheria za uchaguzi zilizotungwa bungeni zinatoa nafasi ya ushindani, kwa hiyo tusibwete, badala yake tujipange vizuri. Tunatakiwa tujipange wanachama ili tupate ushindi wa kishindo mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu mwaka 2025," amesema.

Kinana amesisitiza kuwa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa ni vema wana CCM wakashikamana na kama kuna mtu mchana yuko upande wa CCM na usiku upinzani anapaswa kuwekwa kando haraka.

"Hatuwezi kukubali watu wavae nguo za kijani mchana halafu baadaye unabadilika, hatuwezi kukubali," amesema Kinana ambaye pia ni Mlezi wa CCM Mkoa wa Mara.

Aidha, amesisitiza umoja na mshikamano na kama kuna changamoto zozote wanapaswa kuzizungumza kama Chama kupata ufumbuzi wake. "Tunatakiwa tushikamane na tuzingatie kanuni na katiba yetu ya CCM."

Kuhusu viongozi ambao wamechaguliwa na sasa wako madarakani wakiwemo madiwani na wabunge, Kinana amesema waachwe wafanye kazi na hakuna sababu ya kuwavuruga.

"Kuna watu wanaitwa madalali wa vyeo, kazi yao ni kuuza vyeo anakuja kwako anakwambia mwaka ujao unatakiwa tukuchague wewe, ukisikia hivyo ujue anatafuta riziki na akimaliza kuzungumza anaomba nauli, ujue huyo ni dalali.

"Wakati mwingine anakupigia simu anakwambia hebu nirushie bando kuna habari nataka nikupe. Hao ni madali, ukija kuanguka anasema mimi nilikusaidia ila wajumbe wamekuangusha." Ameeleza.

Amesema kwa kuwa kipindi cha uchaguzi bado hakijafika na kuna watu wanatamaa ya kuwa madiwani, ingawa jambo hilo si dhambi, lakini ni muhimu utaratibu wa Chama na kanuni mbalimbali ziheshimiwe.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara Abdulrahman Kinana akisalimiana na Mtoto wa Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Madaraka Nyerere, alipofika kuzuru kaburi hilo Mwitongo, wilayani Butiama Mkoa wa Mara akiwa katika ziara ya kuimarisha mkoani humo.

**AKEMEA UKABILA**

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara Abdulrahman Kinana amewasisitiza wanachama wa chama hicho na wananchi kwa ujumla kuachana na tabia za ukabila akieleza kuwa ni mambo ya kizamani na yanawagawa.

Akizungumza na wajumbe wa halmashauri kuu ya CCM Wilaya ya Roria, mkoani Mara, alisema nchi kuwa na makabila ni jambo la kawaida ila ukabila ni jambo baya, akieleza kuwa kumuhukumu mtu kwa jambo ambalo hana uwezo nalo sio sahihi.

Kinana alisema hayo baada ya baadhi ya wajumbe kuibua hoja kwamba kuna mambo yanafanyika katika wilaya ya Roria ambayo yanaashiria kuwepo kwa changamoto ya ukabila miongoni mwao.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara Abdulrahman Kinana akizungumza na Viongozi Wa CCM katika kikao maalumu cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya Rorya mkoani Mara akiwa katika ziara ya kuimarisha Chama mkoani humo.

Alisema Baba wa taifa Julius Nyerere ametoka mkoa huo, na ni kabila dogo sana na ameongoza nchi kwa miaka 24, na kwamba alipendwa, aliheshimiwa, alithaminiwa na alitukuzwa sio kwa sababu ya ukabila bali ni kazi aliyokuwa anafanya, utendaji na uadilifu wake uliomfanya aheshimika Tanzania, Afrika na duniani.

"Sasa usimpe mtu nafasi ya uongozi kwasababu ya kabila lake, dini au umbile usimuhukumu, hayo ni mambo ya kizamani sana, tuangalie mtu anauwezo atafanya kazi atajituma na kujitolea, mnampima kwa vigezo sio kwamba huyu ni ndugu yangu.

"Mtu mmoja kwenye kabila lako akipata cheo anakusaidia nini hasa wewe mwenyewe? Uko kijijini kule mngekuwa mnagawana mshahara sawa, kila mmoja anakuletea 300,000 kutoka kwenye mshahara wake kwasababu ni kabila lako sawa... wekeni watu kwa uwezo," alisisitiza Kinana.

Aidha, alieleza kuwa jambo ambalo Baba wa taifa aliwaachia ni umoja wa kitaifa, akitolea mfano kwamba kuna nchi jirani, hakuzibainisha kwa majina, kwamba mtu hawezi kuwa gavana wa jimbo kama anatoka sehemu nyingine, lakini Tanzania wanafanya kazi nchi nzima.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara Abdulrahman Kinana akiweka shada la maua katika kaburi la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alipofika kuzuru kaburi hilo Mwitongo, wilayani Butiama Mkoa wa Mara akiwa katika ziara ya kuimarisha mkoani humo.

# Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi katika picha tofauti akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Songwe
















Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Aprili 17-23, 2024 |




Jarida hili haliuzwi



# Timu Nchimbi kila la kheri, mmeanza vizuri

UK. 12 & 13



# Sisi ni wapekee kwa Muungano wa kipekee duniani

Na Hamid Yassin

NDANI ya miaka mitatu tu ya uhuru chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Tanganyika iliungana na Zanzibar na kuzaliwa taifa la Tanzania. Kuanzia hapo rasmi jina la Tanganyika likafutwa na upande huu wa pili wa muungano ukaanza kujulikana kama Tanzania Bara.

Mkataba ule wa Muungano ulitiwa saini na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, hayati Mwalimu Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume Aprili 22, 1964 huko Zanzibar.

Ulithibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi hapo Aprili 26, 1964 na ilipofika Aprili 27, mwaka huohuo viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika Ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam na kubadilishana Hati za Muungano.

Sheria za Muungano wakati ule zilitoa tamko la Jamhuri katika Ibara ya 4 ikiwa na maana; Jamhuri ya Watu wa Zanzibar italazimika siku zote baada ya kuungana, kuunganishwa kuwa Dola ya Jamhuri kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (Ibara ya 4 Sheria za Muungano).

Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lilibadilishwa baadaye Oktoba 28, 1964 na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitisha Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Sheria namba 61 ya mwaka 1964.

Uongozi wa Mwalimu Nyerere na Karume uliijengea Tanzania heshima ya kimataifa kutokana na msisitizo wake wa maadili kama msingi wa maamuzi ya siasa.

Tangu Aprili 26 mwaka 1964 ni miaka 60 sasa, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umedumu, bado upo imara, madhubuti na wenye afya. Je, nini siri ya mafanikio ya Muungano huo?

Ni dhahiri utashi, ukomavu na ushupavu wa kisiasa huku vikichagizwa na nia ya dhati waliyokuwa nayo waasisi wa nchi hizi mbili; Mwalimu Nyerere wa Tanganyika na Karume wa Zanzibar.

Muungano huu ni wa kipekee kwani umefanya wananchi wa pande mbili zote za Muungano kuishi na kupendana kindugu licha ya tofauti zao za kidini, kiitikadi na kikanda. Hili ni jambo la kujivunia sana kwani nchi mbalimbali zilitamani kufanya hivyo, Afrika na dunia kwa ujumla lakini jambo hili limewashinda wengi.

Licha ya changamoto na tofauti ndogondogo zilizopo katika Muungano, bado Watanzania wamebaki wakiwa kitu kimoja, wakiishi kwa utulivu na amani.

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni mmoja wa kutolewa mfano miongoni mwa majaribio mengi ya nchi na nchi kuungana duniani ambapo wengi hawakudumu. Kwa uchache tu, leo Muungano wetu unatukumbusha baadhi ya mataifa yaliyojiunga na juhudi zao kugonga mwamba kutokana na changamoto mbalimbali.

Upekee wa Muungano huu pia unatokana na muundo wa wake, wengine wanasema ni shirikisho, wengine wanasema ni muungano. Moja ya mambo yanayowasumbua wasomi wa katiba na sayansi za siasa ni aina ya Muungano wetu ambapo ziliungana nchi mbili ikazaliwa nchi moja lakini yenye serikali mbili.

Muungano wetu una upekee kimuundo kwa sababu kuna serikali mbili kwa maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ina mamlaka katika Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo ina mamlaka ndani ya Zanzibar pekee.

Serikali hizi zinaendesha mambo yake bila kuathiri upande mwingine lakini pia zinatumia sarafu moja, lugha moja na uwakilishi mmoja kimataifa na kuufanya Muungano huu uzidi kuonekana wa kipekee.

Akiongea kuhusu Muungano huu katika mahojiano maalumu na Kituo cha Televisheni cha NTV cha nchini Kenya, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete alisema; "Muungano huu kuendelea kuwepo kwa zaidi ya nusu karne ni mafanikio makubwa. Kumekuwepo na wakati mgumu na changamoto mbalimbali, lakini tumeweza kukabiliana nazo na umeendelea kuwa imara zaidi. Siyo kuendelea kuwepo tu pia umeendelea kuimarika."

Dk. Kikwete alitolea ufafanuzi zaidi kuhusu kudumu na upekee wa Muungano akisema pia umefanikishwa kwa kutatuliwa kero. Mwaka 2006 kero za Muungano zilikuwa zimebaki 13 kati ya 31 zilizowasilishwa na Tume ya Shelukindo. Baadaye kero tisa zikafanyiw kazi na kukabaki kero nne tu.

Duniani zimekuwepo jitihada za kuunda Muungano wa mataifa mbalimbali lakini jitihada hizi ama zilifanikiwa kwa kipindi kifupi au ziliishia njiani. Mwaka 1922 uliundwa Muungano wa Kisovieti wa Kisoshalisti wa Urusi, ukijumuisha nchi wanachama 15.

Muungano huu ulidumu kwa takribani miaka 69 na kuvunjika Disemba 26, 1991 kutokana na kushindwa kufikiwa malengo ya Umoja huo.

Siyo Muungano huo tu wa Kisovieti bali kulikuwa na majaribio mengi ya Muungano yalifanyika barani Afrika na kwingineko duniani lakini yalishindwa kudumu.

Historia ya kuundwa Muungano wa nchi au shirikisho katika nchi za Kiafrika inathibitisha kuwa kulikuwa na majaribio mengi lakini yalishindwa.

Mapema miaka ya 1960 jaribio la kuunganisha Mali, Ghana na Guinea lilishindikana. Liberia, Ghana, Guinea na Mali waliunda Muungano lakini jaribio hilo ilivunjika mwaka 1962.

Shirikisho la nchi za Misri, Libya na Sudan liliundwa mwaka 1970 na kufa mwaka 1971. Shirikisho lingine la Misri, Libya na Syria liliundwa mwaka 1972 na kuvunjika mwaka 1977. Muungano wa Misri na Libya uliundwa 1972 na kuvunjika 1974.

Muungano mwingine ni wa Misri na Syria wa mwaka 1962 hadi 1977. Mwaka 1982, Senegal na Gambia waliiungana na kujiita Senegambia nao haukufika popote.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipoundwa mwaka 1964 kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (inayojumuisha Visiwa vya Pemba na Unguja), Tanganyika ilikuwa imetoka kutawaliwa wa Waingereza chini ya udhamini wa Umoja wa Mataifa (UN) huku Zanzibar yenyewe ikiwa imejiondoa kwenye makucha ya Sultani.

Katika mkutano na Waandishi wa Habari, Ikulu, Oktoba 29, 1964, Rais Nyerere alitangaza kwamba, Baraza la Mawaziri limechagua jina "Tanzania" kuwakilisha Jamhuri ya Muungano, akiwafundisha pia namna ya kulitamka jina jipya, kwamba ni "Tan-Zan-ia", sio "Tanzania".

Tanzania ni kifupisho chenye kumaanisha Tan – Tanganyika na Zan – Zanzibar, ambapo herufi – "ia" kukamilisha Tan-zan-ia, zimetoka Zanzibar (i) na Tanganyika (a). Kati ya majina manne yaliyochuana hadi mwisho na "Tan-Zan-ia", ni pamoja na "Tanzan", "Tangibar" na "Zantan".

Ni ukweli usiopingika kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioizaa Tanzania ni wa kipekee kimuundo pia umedumu muda mrefu na unaendelea kudumu licha changamoto chache ulizopitia.

Ukiwa unafikisha miaka 60, tuendelee kuulinda na kuutetea Muungano huu.



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Waandaaji tuzo ya uandishi bunifu mnaweza kuchukua ushauri huu

Nianze kwa kuishukuru na kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuanzisha Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu. Na hasa pongezi zangu za dhati zimwendee Waziri wa Elimu, Profesa Adolf Mkenda aliyekuja na wazo hili na kulisimamia mpaka limezaa matunda.

Ni wazo zuri kwa sababu ya faida zake ambazo ni pamoja na kuamsha ari ya Watanzania kuandika vitabu katika nyanja mbalimbali za fasihi kama vile riwaya, hadithi za watoto na mashairi.

Ni hatua inayosaidia kuongeza idadi ya vitabu vya fasihi shuleni na kwenye maktaba zetu, kukuza Lugha adhimu ya Kiswahili, kusaidia waandishi wa Tanzania gharama za kuchapa vitabu, kusaidia wachapishaji binafsi na faida nyingine kadha wa kadha ikiwemo ya kuendelea kumwenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye alikuwa mwanafasihi.

Ninawapongeza pia waandaaji wa tuzo za mwaka huu kwa jinsi mambo yalivyokuwa mazuri Jumamosi ya Aprili 13, 2024. Baadhi ya mambo hayo ni kumleta mgeni rasmi sahihi kabisa, Mshindi wa Tuzo ya Nobel kwa upande wa Fasihi, Profesa Abdulrazak Gurnah, Mtanzania anayeishi Uingereza; Ukumbi murua uliopambwa vyema na shughuli nzima kuendeshwa vizuri mwanzo mwisho.

Pia ninawapongeza wote walioshinda tuzo, Laura Pettie Kissakwa kwa upande wa Riwaya, Mohammed Omar Juma kwa upande wa mashairi na Blandina Isabella Lucas kwa upande wa hadithi za watoto.

Nawapongezea pia wote walioingia kwenye kumi bora na kila aliyethubutu kushiriki hata kama hakutajwa kabisa kwenye kumi bora, asikate tamaa. Mwakani ajaribu tena.

Ninafahamu kuna watu walituma miswada yao mwaka jana na mwaka huu lakini haikubahatika kuingia kwenye kumi bora. Hawa pia ninawaomba wasikate tamaa. Wajitahidi kufuata vigezo kama vilivyoainishwa wakati wa utoaji wa tuzo na kuhakikisha miswada yao inapitiwa na wahariri ili kuiboresha.

Mambo ya kupongeza katika hizi tuzo ni mengi lakini kwa leo, nimalizie kwa kupongeza hatua ya kubadili au kuchanganya majaji. Kama sikosei katika jopo la majaji wa mwaka huu kulikuwa na sura mpya kwa maana kwamba miongoni mwao kama si wote, si wale wa mwaka jana.

Nasema hivyo kwa sababu kazi ya kujaji fasihi andishi ambazo si mahesabu kwamba jibu ni moja, licha ya kuweka vigezo, wakati mwingine mrengo, mtazamo, itikadi, upenzi wa jaji pia una nafasi katika kuamua riwaya ipi, hadithi ipi ya watoto au shairi lipi lichukue nafasi gani.

Kwa mfano, mimi kati ya riwaya ambazo ukinipa inanishinda kusoma (kama si hadithi ya watoto) ni yenye matukio au masimulizi ya kufikiria kama vile: "Ghafla likatokea jini, likammeza yule adui huku nikishuhudia", au "kutokana na uchawi aliopewa na babu yake, walipomkaribia akapaa. Akawa anaruka kutoka ghorofa moja kwenda jingine" na mengine mfano wa hayo. Lakini kuna wapenzi wa riwaya za aina hiyo!

Labda katika hili nishauri tu kwamba, wakiona inafaa, pale kwenye jopo la majaji wanaweza kuingiza hata mabingwa wa kusoma vitabu kwani baadhi wanafahamika. Ninawafahamu watu wanne ambao wamejipambanua kama wasomaji wakubwa wa vitabu nchini kama Buinda Mujungu wa pale Arusha, Peter Chapusa wa Bagamoyo, Salim Aljabry wa Dar es Salaam na mwanasiasa Zitto Kabwe.

Huyu mwamba, Chapusa, alinishangaza siku moja aliponiambia ana vitabu zaidi ya 400 kwenye maktaba yake nyumbani. Lakini alinishangaza zaidi alipoanza kunitajia mtunzi gani kaiba hadithi ya nani!

### KUSHIRIKI ZAIDI YA NYANJA MOJA

Mmoja wa magwiji wa uandishi bunifu ambao nchi hii imewahi kuwashuhudia ni Hayati Shaaban Robert. Hili gwiji lilikuwa mahiri katika riwaya, insha na mashairi.

Leo Shaban Robert angekuwepo, halafu kwenye tuzo hii ya uandishi bunifu ukambana kwamba ashiriki nyanja moja pekee, kama anachagua mashairi, asiguse riwaya au hadithi za watoto na kinyume chake, asingekuelewa.

Hata sasa, Alhamdulillah, tunao akina Shaaban Robert kadhaa na mmoja ninayemfahamu ni Katibu wa Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira (UWARIDI), Ibrahim Gama. Pia ninawafahamu watu kama Lilian Mbaga ambaye ni mtunzi mzuri wa riwaya kwa ajili ya watu wazima na hadithi za watoto.

Moja ya masharti ya mashindano haya ni mtu kuchagua nyanja moja tu. Mimi sioni kama ni vibaya mtu kama anaweza nyanja zaidi ya moja kwa nini asijaribu kotekote. Na pengine siku moja tunaweza kuona mtu akishinda nyanja zaidi ya moja kama ambavyo niliona kwenye mashindano ya masuala ya filamu mwaka huu.

**Huyu mwamba, Chapusa, alinishangaza siku moja aliponiambia ana vitabu zaidi ya 400 kwenye maktaba yake nyumbani. Lakini alinishangaza zaidi alipoanza kunitajia mtunzi gani kaiba hadithi ya nani!**

### VITABU AINA HII VIRUHUSIWE PIA

Katika mashindano ya mwaka huu ya kuwania Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kulikuwa na masharti ya muswada usiwe umechapishwa na mchapaji (anayefahamika), usiwe umechapwa na mwandishi binafsi au kuchapishwa mtandaoni.

Kama moja ya malengo ya kuanzisha tuzo hii ni serikali kusaidia waandishi wa Tanzania kuchapa vitabu vyao kwa kuwa gharama ni kubwa na pia kuongeza idadi ya vitabu vya fasihi ya Kiswahili kwenye mashule na maktaba zetu, sharti hili linapaswa kuangaliwa upya kama nitakavyojadili.

Kuna watu wamekuwa ni miswada mizuri lakini wanapata ugumu kwenye kuichapa, sababu kubwa ikiwa ni fedha. Wakitaka ithibati ya Baraza la Kiswahili wanaambiwa milioni kadhaa za pesa ambazo hawamudu na hata wakienda Taasisi ya Elimu (TET) ili kuona kama vitabu vyao vinaweza kuingia kwenye mitaala pia wanakutana na gharama. Hawa wakienda kwenye kampuni za uchapishaji wanakutana na urasimu na/ au kuambiwa malipo ya mirabaha ambayo haiwaridhishi.

Baadhi ya hawa wameingia pale Kariakoo na kuchapa riwaya zao, mashairi au hadithi za watoto nakala chache sana, mara nyingi hazizidi 1,000 ili angalau 'watoke'. Vitabu hivi mara nyingi vinachapwa bila ubora wala ithibati yoyote licha ya kuwa na maudhui bora.

Nimebahatika kusoma vitabu kama Fumbo cha Maundu Mwingizi, Bondia cha Hussein Tuwa, Kiroba Cheusi cha Laura Pettie, Hatinafsi cha Lilian Mbaga na vinginevyo.

Kwa mtazamo wangu, riwaya kama hizi zingeruhusiwa kushiriki kwani baadhi zikishinda tuzo na kwenda kwenye mlolongo 'unaoeleweka' zitaongeza kitu katika fasihi ya Tanzania kuliko kuziacha huko 'vichakani' ziliko ambako hata kama zimekwisha kabisa madukani, wahusika wanaweza kuchukua miaka kadhaa wakitafuta pesa kuvirudufisha nakala nyingine.

Pengine walioweka sharti hili, wanalinganisha waandishi wengi wa Tanzania na watu wenye uwezo wa kuchapa vitabu vyao hata nje ya nchi! Wengi, nikiwemo mimi tuna riwaya tunazodhani ni nzuri lakini zimechapwa vichochoroni na ziliwafikia Watanzania wasiozidi 1,000 kati ya Watanzania zaidi ya milioni 55!

### MAJAJI KUELEZA MAKOSA WALIOONA

Katika tuzo za mwaka huu, niliona majaji wakieleza vigezo walivyokuwa wakifuata lakini pia wangeweza kueleza makosa yaliyofanywa na wengi katika kila nyanja ili kuwajenga watakaoshiriki mwaka kesho wasirudie makosa yaleyale. Nashauri hili walifanye tuzo zijazo.

Pamoja na kupatikana washindi wa kila nyanja nina hakika mshindi hawezi kuwa sahihi asilimia 100 kwa sababu si malaika. Ni katika muktadha huo, nashauri ingekuwa vizuri majaji hawa kukaa meza moja na kuwaeleza washindi maeneo ya kuboresha, hata kama ni machache, kabla ya muswada kuchapwa kitabu.

### KUONGEZA WIGO VITABU VYA KUCHAPA

Mambo ni mengi ya kushauri. Nitaendelea siku nyingine lakini leo nimalizie kwa kushauri serikali kupanua wigo wa vitabu vya kuchapa.

Ningetamani kuona angalau vitabu vitatu; yaani cha mshindi wa kwanza hadi wa tatu kwa kila nyanja vinachapwa na serikali na kama bajeti inabana basi angalau viwili.

Lakini ninaamini kampuni za uchapaji zitafanyia kazi pia ushauri uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo, Profesa Penina Mlama ambaye alizitaka kuingia mikataba na washindi kuanzia namba moja hadi 10 ili kuchapa vitabu vyao. Hili limekaa vizuri sana. Hapa pia serikali inaweza kufikiria kuwapa ruzuku wachapishaji.

Kwa kumalizia, nashauri ikiwezekana, washindi kuanzia namba nne hadi 10 wasiishie kupata tu cheti bali fedha, hata kama ni lakini tatu kila mmoja ili 'kuwafuta' jasho na kuhamasisha zaidi ushiriki tuzo zijazo.

Hili linawezekana kwa kupunguza gharama za maandalizi. Kwa mfano, ningekuwa mimi ningealika mgeni mmoja mmoja tu kutoka Kenya na Uganda badala ya kuleta zaidi ya mmoja, labda kama wanajilipia gharama!

### LAURA MSHINDI WA RIWAYA TUZO YA MWL. NYERERE

Laura Pettie Kissakwa wa Dar es Salaam ameibuka mshindi wa kwanza kwenye kipengele cha Riwaya katika Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunugu iliyotolea usiku wa Aprili 13, 2024 katika ukumbi wa The Super Dome Masaki Dar es Salaam.

Hata hivyo, Laura, mwandishi wa kitabu maarufu cha Kiroba Cheusi hakuwepo ukumbini na hivyo tuzo ilipokelewa kwa niaba yake na Mwalimu Kalunga Matovolwa kutoka Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira (UWARIDI).

Katika hafla huyo mgeni rasmi alikuwa Profesa Abdulrazak Gurnah ambaye ni mshindi wa Tuzo ya Nobel ya mwaka 2021 katika Fasihi.

# Timu Nchimbi kila la kheri, mmeanza vizuri

**Na Hamid Yassin**

TAFSIRI sahihi ya neno 'chama' kwa mujibu wa Kamusi yetu ya Kiswahili ni kikundi cha watu waliooungana pamoja kwa lengo la kutekeleza matakwa yao ya kisiasa, kiuchumi, kijamii n.k; hivyo kamwe hakiwezi kuendeshwa kwa nguvu, uwezo, akili, maono na hata amri na maamuzi ya mtu mmoja!

Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi (CCM) chini ya uongozi wa Katibu wake Mkuu, Dk. Emmanuel Nchimbi Aprili 13 ilianza ziara ya awali ya mikoa sita kule mkoani Katavi na karibu viongozi wote walioongea walihimiza suala la umoja na mshikamano miongoni mwa Wana- CCM na Watanzania kwa ujumla.

Katika hotuba yake pale Katavi, Dk. Nchimbi amesema Watanzania wana imani kubwa na CCM, hivyo ni wajibu wa kila kiongozi kushughulika na kutatua kero zao.

"CCM ni chama cha kupigania haki ya wanyonge na lazima tuendeleze hilo katika kila ngazi kuanzia shina hadi taifa, wananchi wana imani kubwa na CCM hivyo ni wajibu wa kila kiongozi kushughulikia kero, adha na masaibu ya wananchi wetu," alieleza Dk. Nchimbi huku akisisitiza hilo si jukumu la kiongozi fulani au mtu mmoja.

"Katika miaka mitatu, serikali ya CCM chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imefanya mambo makubwa sana. Msione haya kuyatangaza na kuyasemea, siasa ni lazima useme ulichofanya bila kusema hata aliyeshuhudia ukifanya atajifanya kama hajaona, wengine watasema bana si wajibu wenu kufanya, yaani atachukulia kirahisi na bila kujali, lazima tuisemee vema serikali yetu inayowajali wananchi wake kwa kuwa ni serikali inayojitambua," Dk. Nchimbi alizidi kutoa darasa la bure.

Pia aliwataka Wana-CCM kote nchini kujitokeza hadharani kifua mbele kutetea serikali ya chama chao huku akiwataka wale wenye tabia ya kujikweza na umimi, waache mara moja wanaposimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM, wasitafute maslahi binafsi, sambamba na kuacha tabia ya kuwafuata viongozi wa serikali, kuomba fedha kwa kuwatisha na kuweka uongo ndani yake.

Dk. Nchimbi amefichua kuwa, wapo viongozi wa CCM wenye tabia hiyo na wanawajua na kusisitiza hiyo si haki bali ni ukandamizaji na wizi, kisha akawaagiza watumie wajibu wao wa haki kama wana CCM.

Balozi Nchimbi pia aliwaambia Wana - Katavi kwamba wamesikia kero zao hususani ile ya umeme na kuahidi kwamba wanakwenda kuitatua kwa kasi kama alivyowaeleza Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amosi Makala ambaye alitangulia kuongea katika mkutano huo wa hadhara.

Naam, hii ndiyo CCM ninayoijua mimi, hii ndiyo misingi ya chama hiki iliyowekwa na waasisi wake, na siyo hii tabia inayozuka siku hizi kwa baadhi ya viongozi kuota mapembe na kujifanya wao ndiyo chama, wao ndiyo alfa na omega; yaani wanataka kuwaaminisha watu kwamba bila wao hakuna CCM! Hii kamwe haiwezekani na haikubaliki!

Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere wakati anastaafu alisema, namnukuu; "Mimi nang'atuka lakini naendelea kuamini kuwa bila CCM madhubuti nchi hii itayumba." Hivyo niwaambie ndugu zangu mtu asiyeitakia mema nchi hii atatamani kuona CCM inapasuka.

**ITIKADI**

Kwa miaka mingi, CCM imekuwa ikifuata itikadi ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Itikadi hii ilipewa nguvu za kisera mwaka 1967 pale lilipotangazwa Azimio la Arusha. Kutokana na azimio hilo uchumi uliwekwa mikononi mwa umma sambamba na kusisitiza umuhimu wa kushirikiana miongoni mwa raia.

Ni wazi Dk. Nchimbi na timu yake wameliona hili. Hivyo wamedhamiria kukirudisha chama katika misingi yake ya awali, naamini ikiwemo kuitekeleza kwa vitendo siasa ya ujamaa na kujitegemea kwa mazingira ya sasa.

Tunataka kila linalofanywa na chama hiki pamoja na serikali yake, liendane na imani ya ujamaa na kujitegemea.

Katika mkutano ule wa kwanza katika ziara ya Sekretarieti hiyo mpya ya CCM kule Katavi, pia Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amosi Makalla aliwataka watu wajue kuwa mambo yaliyo mahakamani yanamalizwa mahakamani na hakuna kiongozi wa Serikali au Chama anayeweza kuingilia Mhimili wa Mahakama.

"Mimi nimetoka kwenye ukuu wa mkoa. Ninaposikiliza kero, kwanza huwa tunasikiliza kero ambazo hazipo mahakamani, siku moja nipo Mbeya kuna mtu alikuja na makabrasha akasema Mahakama ya Kwanza alishindwa, Mahakama ya Wilaya alishindwa, Mahakama Kuu alishindwa, Mahakama ya Rufaa pia alishindwa, akaniambia wewe umeteuliwa na Rais tengua hizo hukumu zote, ingewezekana vipi?" Alihoji Makala.

"Lazima watu wetu wajue mambo yaliyo mahakamani yanamalizwa mahakamani. Tunachoweza kukupa ni ushauri basi, sisi tunawasaidia wananchi yale mashauri ambayo yanahitaji mambo ya utawala, kwa hiyo mkija kwenye mkutano wa hadhara tunawakaribisha, lakini msilete mambo ambayo yapo mahakamani. Ukweli lazima usemwe, itakuwa tunawadanganya tu watu kuwaambia kwamba tunaweza kuwasaidia masuala yaliyopo mahakamani, sio kweli. Lazima wakati mwingine tuseme kweli."

Huu ndiyo utawala wa sheria unavyotakiwa kuwa. Siyo kiongozi unawaambia wananchi kama hamna fedha msiende kudai haki mahakamani kwani huko ni kwa matajiri na siyo watu maskini!

Inasikitisha, hapa kiongozi si tu anauchafua Mhimili wa Mahakama bali pia hamtendei haki kiongozi mkuu wa nchi aliyemwamini na kumpa hayo madaraka!

Viongozi ni kioo cha jamii, hivyo kila linalokutoka ulimini linatakiwa liwe lenye busara, kujenga na kuelimisha mbele ya jamii unayoiongoza.

**CCM HAITAKIWI KUGAWA WATU**

CCM ni chama kikongwe na chenye uzoefu mkubwa hivyo kamwe kupitia viongozi wake hakitakiwi kuchafua holela taasisi zake wala kugawa watu kwa kuwa hilo linasababisha mpasuko wa ndani ya chama, kunakwamisha maendeleo kwa wananchi sambamba na kuwapa faida wapinzani wake kupata mianya ya kuwaponda kwenye hadhara zao.

Nimefurahishwa na kauli ya Dk. Nchimbi kuliona hilo, kwamba Chama Cha Mapinduzi hakitaki na kinakemea tabia ya uongozi wa kugawa watu kwa kuwa unapelekea mpasuko ndani ya Chama na kukwamisha maendeleo kwa Watanzania.

Balozi Dkt. Nchimbi amebainisha kuwa moja ya changamoto kubwa iliyopo ndani ya CCM ni



tabia ya baadhi ya viongozi wanaoshindwa na wale wanaoshinda katika chaguzi kutokukubali matokeo moyoni mwao na matokeo yake, pamoja na uchache wao, wamekuwa na madhara makubwa kwenye muktadha wa maendeleo ya chama na kutaka tabia hiyo iachwe mara moja kwa kuwa ni ujinga na sio misingi ya demokrasia.

"Unakuta mtu kagombea na kashida lakini baadaye anaibuka na kuanza kutafuta nani hakumuunga mkono ili apambane naye na kumkandamiza, hiyo ni tabia ya kijinga na haiungwi mkono. Tuache mara moja," ameonya Balozi Dkt. Nchimbi.

**MFUMO WA VYAMA VINGI**

Miaka hairudi nyuma na Tanzania siyo kisiwa, mabadiliko ya yaliyotokea duniani baada ya kumalizika kwa vita baridi kati ya Mashariki na Magharibi, ikabidi na nchi yetu mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini urudi mwaka 1992.

Kurudishwa kwa mfumo huu kulitokana na taarifa ya Tume ya Hayati Jaji Francis Nyalali, iliyopewa kazi ya kuhuisha mfumo wa siasa nchini kufuatia mabadiliko hayo yaliyojiri duniani.

Katika taarifa ya Jaji Nyalali, wananchi walipoulizwa kuhusiana na mfumo wa vyama vingi kurudishwa hapa nchini, asilimia 20 tu ndio walikubaliana nao na asilimia 80 wakasema tuendelee na mfumo wa chama kimoja.

Hata hivyo, Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM pamoja kwamba iliona Watanzania wengi walitaka kuendelea na chama kimoja, wakaamua kukubaliana na kundi dogo lililoutaka mfumo huu.

Kukubaliwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, kukafungua ukurasa mpya kisiasa nchini. Makundi ya watu waliokuwa wakiendesha harakati za kutaka mageuzi nchini, sasa yakawa huru kuanzisha vyama vya siasa.

Hapa tukaanza kushuhudia zilizokuwa kamati za mageuzi zikiwa vyama vya siasa na mfano mzuri ni NCCR-Mageuzi.

Tukashuhudia KAMAHURU kutoka Zanzibar chini ya marehemu Seif Shariff Hamad ikiungana na Chama cha Wananchi (CWT) cha marehemu James Mapalala kutoka bara wakaunda Chama cha Civic United Front (CUF).

Vyama vikaendelea kuundwa kama vile Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) chini ya Edwin Mtei, Tanzania Labour Party (TLP) chini ya Leo Lwekama, NRA chini ya Ahmad Olotu, NLD chini ya marehemu Emmanuel Makaidi, UMD chini ya marehemu Mzee Said Fundikira, UDP chini ya John Cheyo na UPDP ya Fahmi Nasoro Dovutwa.

Vingine viliendelea kuanzishwa na kupewa usajili wa kudumu na kuingia kwenye uwanja wa siasa.

Kwa bahati mbaya, vyote hivi viliingia vikiwa vigeni katika kufanya siasa zaidi ya uana harakati. Ungeweza kufikiria kuwa, huenda waanzilishi walikuwa na uzoefu katika nyanja ya siasa, lakini ukweli ni kwamba, idadi kubwa ilikuwa ya wanasiasa wasio na uzoefu.

Hata kama walikuwapo waliofahamika huko nyuma wakiwa katika chama cha TANU na baadaye CCM kama vile, marehemu Mzee Fundikira, marehemu Seif, marehemu Shaaban Mloo, na wengine wachache, lakini walishindwa kuendana na dhana halisi ya siasa. Walikuwa na viongozi wenzao ambao wengi wao walikuwa ni wanaharakati tu.

**TOFAUTI YA CCM NA VYAMA VINGINE**

Kuna tofauti kubwa kati ya CCM na vyama vingine vya siasa nchini. Tofauti kati ya CCM na vyama vingine zipo nyingi, lakini nitazijadili chache tu.

Kwanza kabisa, tofauti kubwa ni kwamba, CCM ndio chenye Serikali tangu mwaka 1995, tumezoea kukiita chama tawala. Ndiyo chenye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Spika wa Bunge la Tanzania, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Waziri Mkuu, Waziri Kiongozi, na Mawaziri.

Kutokana na ukweli kwamba CCM ni chama tawala, hutegemei basi viongozi wa CCM, ambayo ndio wenye Serikali wakawa wazushi, waongo, wachochezi, wafitini, wabaguzi ndani ya chama kama walivyo baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani.

Viongozi wa CCM wawe wafitini ili iweje, waseme uongo ili wapate nini, wawachochee wananchi kufanya vurugu kwa faida ya nani? Serikali ya CCM imekula kiapo baada ya kupata ridhaa ya wananchi, hivyo hatutegemei kusikia kutoka midomo ya viongozi wao maneno yasiyo kichwa wala miguu. Wakati wote wapo makini kwa sababu wapo kuwatumikia. Na ndio maana Dk. Nchimbi anasema wananchi wa imani kubwa na CCM

Tofauti nyingine ni kwamba, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ndio imekubaliwa na Watanzania hivyo ni kazi yake kuona Serikali zake zinatekeleza Ilani zake za Uchaguzi tangu mwaka 1995 hadi mwakani 2025. Vyama vingine hawana. Ilani zao zimekuwa zikikataliwa na Watanzania.

Kazi ya CCM ni kuhakikisha ahadi zake kupitia Ilani ya Uchaguzi zinatekelezwa katika ngazi zote. Katika kipindi chote cha miaka mitano, CCM ina kazi ya kufanya kuhakikisha inasukuma na kuhamasisha maendeleo ya wananchi kama ilivyoanza kazi hii Sekretarieti yake mpya chini ya Komredi Nchimbi na timu yake!

Hatutaraji kuona wala kusikia viongozi wa CCM wakizunguka nchi nzima kupigana vijembe wenyewe kwa wenyewe ama dhidi ya viongozi wa upinzani kama wanavyofanya baadhi yao, uongo na kuchochea chuki miongoni mwa Watanzania.

Kama alivyosema Dk. Nchimbi kila Mwana- CCM anatakiwa kukipambania chama na Serikali yake, kutoka kifua mbele bila woga na kuyaweka hadharani yote mazuri yanayofanywa na chama na Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dk. Samia Suluhu Hassan.

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888787/ 0784 122 020.*








# Zijue faida za ukwaju kwa afya ya binadamu





UKWAJU unajuulikana zaidi kwa matumizi yake kwenye vyakula hasa katika maeneo ya Asia, Amerika Kusini, visiwa vya Caribean na Afrika.

Vilevile, ukwaju ni maarufu katika uponyaji. Hutumika kupunguza maumivu, kutuliza usumbufu wa tumbo na kutuliza homa.

Watafiti wa zama hizi, wamegundua kuwa ukwaju unaweza kutoa faida zaidi za kiafya kuliko ilivyokuwa inajulikana hapo awali.

Katika dawa za jadi, ukwaju umetumika kutibu matatizo yanayohusiana na ini. Ulaji wa ukwaju pia hutumika kutuliza kichefuchefu.

Ukwaju unatoa kinga ya mwili kwa kuzalisha virutubisho vya procyanidins na wataalamu wanaamini vinalinda ini na kukabiliana na magonjwa ya ini.

## AFYA YA MOYO

Kama matunda mengi ya rangi nyeusi, ukwaju una virutubisho vingi vya polyphenols na flavonoids. Virutubisho hivi vinajulikana kuwa na athari chanya kwenye viwango vya mafuta.

Kutumia ukwaju kunaweza kusaidia katika kuvunjika na kupunguza mafuta katika damu. Kusawazisha viwango vya mafuta kunaweza kusaidia afya ya moyo na mishipa kwa ujumla.

## KUPAMBANA NA SARATANI

Virutubisho vya ukwaju, vinaweza kuzuia uharibifu wa seli. Vinaweza kukabiliana na athari za molekuli, ambazo zinahusishwa na mabadiliko ya seli ambayo yanaweza kusababisha saratani.

Ukwjau hutoa kinga nyingi kwa mwili. Katika utafiti kwa wanyama, watafiti waligundua virutubisho vya ukwaju vinaweza kupunguza uharibifu unaosababishwa na saratani wa seli za figo.

Kupambana na maambukizi

Ukwaju hutumika kuondoa maambukizi, hutumiwa kama dawa ya kutuliza maumivu ya majeraha. Kadhalika, ukwaju hupunguza uvimbe na maumivu kwenye jeraha.

Watafiti wamegundua unaweza kupunguza uvimbe wa ndani pia, jambo ambalo lina faida kiafya.

## KUPAMBANA NA KISUKARI

Ukwaju una virutubisho ambavyo vinaweza kuboresha udhibiti wa sukari ya damu kwa wale walio na ugonjwa wa kisukari.

Ukwaju unaweza kutumika kama msaada wa lishe na kuunganishwa na dawa za ugonjwa wa kisukari na hurekebisha tishu zilizoharibika.

## FAIDA KWA NGOZI

Matumizi ya ukwaju yanaweza kuwa na faida kwa matatizo ya ngozi, majipu na shida nyingine za ngozi.

Virutubisho vilivyopo katika ukwaju, hutoa kinga kwa mwili na huonyesha ulinzi dhidi ya uharibifu wa ngozi kutokana na mionzi ya jua.

## UKWAJU NI SALAMA KWA KILA MTU?

Kama chakula, ukwaju ni familia ya kunde na hivyo una uwezo wa kusababisha athari ya mzio kwa baadhi ya watu.

Ukwaju unaweza kupunguza viwango vya sukari ya damu na kwa hivyo unapaswa kutumiwa kwa tahadhari ikiwa una ugonjwa wa kisukari. Unaweza pia kusababisha kuharisha ikiwa utatumiwa kwa kiasi kikubwa.

BBC.

# Mkenya anayemiliki hospitali Marekani



CHRISTINE Ouma alisafiri kwenda Marekani mwaka 2001, alipokuwa na umri wa miaka 20.

Kwa sasa anamiliki hospitali katika jimbo la Texas, nchini humo.

Alisomea taaluma ya uuguzi katika chuo cha Houston Community College kilichoko Houston TX, ambapo alikabidhiwa cheti cha LVN mwaka 2008 na kusajiliwa pia katika taasisi ya Excelsior College, Albany, New York, mwaka 2020.

"Jina langu rasmi la usajili ni RN CRNI®, kwa hivyo, hujulikana kama Christine Ouma RN CRNI®," anasema.

Anasema aliasisi kampuni yake ya kutoa huduma za afya mwaka 2018, lakini wakati huo, alikuwa akifanya kazi kwingine, na akaitumia kama mbinu ya kupata mapato ya ziada.

Aliacha kazi ya kuajiriwa Juni 2022, na kujitosa kikamilifu katika utoaji huduma za uuguzi katika kampuni yake inayojulikana kwa jina Healing Bridges Infusion Specialists, ambapo hutoa huduma katika maeneo tofautitofauti, kama vile nyumbani kwa wagonjwa, vituo vya huduma katika ofisi za madaktari, na katika maeneo yanayouza dawa.

"Kilichonitia motisha ni mapenzi yangu kwa uuguzi wa kunywesha dawa, na mwito wa kutoa huduma," anasema muuguzi huyo.

"Niliamua kuhudumu hapa kwa sababu Marekani kwa sasa ni nyumbani, na nina kibali cha kuhudumu. Pia, ni rahisi kwangu kama muuguzi kumiliki biashara hii katika nchi hii, kwa sababu sheria na mwongozo, itifaki na miundo, hata kama ni kali, zimebuniwa, kufanyiwa utafiti, kuandikwa; kwa hivyo, ni salama kuwa mhudumu wa kujitegemea," anaeleza.

Muuguzi huyu anasema hutoa huduma za uuguzi katika maeneo ya Houston, TX na miji mingine iliyoko karibu na maeneo hayo.

Anasema kwamba, shughuli hiyo ni ghali kuanzisha, kwa sababu kuna leseni na stakabadhi ambazo zinatakiwa kutolewa katika Jimbo la Texas, ambazo ni sharti muuguzi awe nazo, kabla hajamgusa mgonjwa.

Ouma anasema kuwa, baada ya kufanya kazi za kuajiriwa katika kampuni saba, alipata kazi ya uuguzi wa kunywesha dawa kwa bahati tu.

"Haikuwa kwa uwezo wangu. Nilifika hapa kwa neema ya Mungu; nikaipenda, nikaitumikia vyema na kuwa bora kwayo, na hapa ndipo tupo sasa," anasema.

Muuguzi huyo anafichua kuwa, alianza shughuli hiyo peke yake, kama mhudumu, na alikuwa akiwaalika wauguzi wenzake kumsaidia wakati alipokuwa akisafiri, na wakawa timu.

Kwa sasa, ana wafanyakazi zaidi ya kumi – watatu wanaoshughulika ofisini na wengine wanaohudumia wagonjwa nje ya ofisi.


Ouma anasema kuwa, wauguzi wanapoenda kuwashughulikia wagonjwa nyumbani, humhudumia mgonjwa mmoja kwa wakati mmoja, lakini wagonjwa wanapotembelea kituo chao cha matibabu, muuguzi mmoja huwahudumia wagonjwa watatu au zaidi, kila mmoja, kwa wakati mmoja.

Anadokeza kuwa, baadhi ya wagonjwa huhudumiwa kwa muda wa dakika 15 tu.

Anaongeza kuwa, kuna mambo fulani yanayochangia idadi ya wagonjwa wanaoshughulikiwa.

Muuguzi huyo anasema kwamba, anapania kupanua biashara hiyo ili kuwahudumia wagonjwa wengi katika eneo la Texas, na katika maeneo mengine Marekani.

***Chanzo: Taifa Leo***



# Kwa nini ni vigumu kupata mpenzi wa kweli nyakaati hizi?

Teknolojia inatupa fursa nyingi mpya za kukutana na watu mbalimbali wakiwemo wapenzi.

Mwandishi David Robson alizungumza na Paul Brunson, mkuu wa utafiti wa Mtandao wa Tinder - ambaye ameandika kitabu kipya cha Find Love: How to Navigate Modern Love and Discover the Right Partner for You.

Tafsiri yake isiyo maalumu inaweza kuwa: Kutafuta Mpenzi: Jinsi ya Kutafuta Mapenzi ya Kisasa na Kugundua Mwenza Anayekufaa.

Kupata mpenzi daima imekuwa uamuzi muhimu sana, lakini kulingana na utafiti wa kitabu hiki, Brunson anaamini kutafuta na kudumu na mpenzi katika zama hizi ni vigumu zaidi kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya binadamu.

Sababu moja ni kwamba, kuna aina nyingi za mahusiano kwa sasa. Unaweza kuwa na mke mmoja au mume mmoja au kuna uhusiano wa zaidi ya mtu mmoja au uhusiano wa kuishi pamoja au kuishi mbalimbali.

Kuwepo kwa namna nyingi za mahusiano kunafanya kupata mshirika wa kuendana na lengo lako katika mapenzi kuwa changamoto zaidi.

Pili, ni hulka ya mwanadamu kutaka mambo mengi kutoka kwa wenza wetu. Hapo awali, watu walihitaji mtu wa kusaidia kulinda au kulea mtoto, au kutunza shamba.

Lakini sasa tumefikia hatua ambapo tunataka mpenzi awe amekamilika kitu kitu. Tunataka awe sawa kiakili, awe Mkurugenzi Mtendaji, tunataka awe mzazi bora, tunataka awe hodari kitandani pia.

Kwakweli, watu wengi wamekata tamaa. Lakini watu wengine wanatumia changamoto hizo kwa faida yao. Wanajaribu kubaini kasoro katika uhusiano wao, ili waweze kuuboresha.

### KUTAFUTA MPENZI MTANDAONI

Mwandishi pia alimuuliza Paul Brunson swali hili: "Kwa kuzingatia kazi yako katika Tinder, ni aina gani ya makosa ambayo watu hufanya katika mbinu zao za kuchumbiana mtandaoni?"

Naye akajibu: "Kuna makosa kadhaa. Mtu hafanyi maamuzi mapema kutambua lengo la uhusiano autakao. Kwa sababu kuna aina nyingi za mahusiano.

Sasa tumeunda kipengele kwenye Tinder kinachokuruhusu kuchagua lengo lako la uhusiano. Kwa sababu, ikiwa wewe unatafuta mpenzi wa muda mrefu, lakini mimi natafuta mpenzi wa muda mfupi, na tukiingia kwenye uhusiano, italeta shida.

Tatizo jingine kubwa ni picha. Watu hawaweki picha zao za karibuni, kwa hivyo wanapoonekana siku ya kukutana, picha zao hazifanani na wao walivyo sasa.

Nilipojiunga na Tinder miaka miwili iliyopita, ilibidi nifungue akaunti ili kuona hali ikoje, na niliweka picha ambayo nilipiga miaka 12 nyuma.

Mtu niliyekuwa nikifanya kazi naye huko Tinder alisema Paul, huonekani hivyo. Sote tunafikiri tunaonekana kama tulivyokuwa miaka 10 iliyopita, lakini hatuko hivyo.

Unapaswa kuwa na picha tatu hadi tano - moja inayoonyesha tabasamu la kweli, moja inayoonyesha mwili wako mzima, na baadhi ya picha zako ukifanya kitu ambacho unakipenda.

### TOFAUTI YA VIZAZI

Tunapaswa kuelewa kwamba kizazi cha Z (waliozaliwa kuanzia miaka ya 90), katika jiji au nchi yako kinaweza kuwa tofauti na kizazi cha Z katika jiji au nchi nyingine.

Katika utafiti wetu katika Tinder, tuligundua kuwa kigezo nambari moja cha iwapo mtu anataka kukutana nawe kwa mara ya pili au la, ni jinsi alivyoliwazika alipokuwa na wewe kwa mara ya kwanza.

Ilihali katika vizazi vyote vilivyotangulia, mvuto wa kimwili ulikuwa jambo la kwanza. Katika zama hizi, mvuto wa kimwili ni jambo namba mbili kwa kizazi cha Z.

***Chanzo: BBC***

Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Wahudumu wa afya ngazi ya jamii tunawategemea sana



"Mtu ni Afya, Jali Afya Yako", huo ni msemo maarufu unaotumiwa na maofisa wa Wizara ya Afya kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutunza afya zao kwani afya ni mtaji muhimu katika maisha ya mwanadamu hasa katika kufikia mipango na maendeleo endelevu.

Kutokana na umuhimu wa afya bora kwa wananchi, serikali imekuwa ikisisitiza sana wananchi wake kuwa na utaratibu au utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara ili kama kuna tatizo la kiafya ligundulike mapema na kupatiwa tiba stahiki.

Kuna magonjwa kama saratani, tunaambiwa yanatibika kama mgonjwa atagundulika ugonjwa ukiwa hatua ya kwanza au ya pili. Lakini wengi tatizo linakuja kugundulika tayari ugonjwa ukiwa hatua ya nne ambayo ni ya mwisho kabisa. Hapo huwa ni kusubiria tu miujiza ya Mwenyezi Mungu!

Kimsingi, serikali inawajbika moja kwa moja kuhakikisha afya na maisha ya wananchi wake yanakuwa salama. Kutokana na wajibu huu wa serikali kwa wananchi wake, suala la kuwafikishia wananchi huduma bora za afya bila kujali umbali au maeneo wanayoishi halikwepeki.

Ndiyo maana ujenzi na ukarabati wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mkoa, na zile za rufaa unaendea nchi nzima. Vilevile, sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika kujenga na kuboresha vituo vya afya na hospitali ili kasi ya kuwafikishia wananchi huduma bora iongezeke kwa ustawi wa wananchi na maendeleo ya nchi.

Utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi hauwezi kufanikiwa kama hakutakuwa na raslimali watu wa kutosha wa kuhakikishia utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Ndio maana serikali inaendelea na utaratibu wa kuajiri wataalamu wa afya bila kusahau mpango wa kutoa mafunzo na hatimaye kuajiri wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi popote walipo.

Ikumbukwe kuwa moja ya vipaumbele sita vya kisera vya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025 ni pamoja na kuajiri wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili kuwafikishia wananchi huduma bora kule walipo.

Januari 31, 2024 kulifanyika tukio la Uzinduzi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii. Uzinduzi huo ulifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam ambapo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alisema katika kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi kuanzia katika ngazi za chini kabisa, serikali imetenga shilingi bilioni 899.4 kufanikisha azma ya kuwajengea uwezo jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao 137, 294 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

"Wahudumu wa afya mtakaopewa dhamana ya kutekeleza jukumu hili zingatieni weledi na kujituma pamoja na kutoa rai kwa jamii kupokea mpango huu na kuthamini huduma za wahudumu wa afya ngazi ya jamii kwa kuwapa ushirikiano wa kutosha ili kulinda na kuboresha afya katika jamii," anasema Dk. Mpango.

Kusudio la serikali la kutumia mabilioni hayo ya pesa kwa ajili wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni katika kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa na huduma za afya ili kuimarisha afya za wananchi wote.

Ndiyo, wahudumu hawa watakuwa na jukumu la kutoa elimu ya afya, huduma za afya kinga, huduma tembezi na mkoba na baadhi ya huduma za awali za tiba kabla ya kutoa rufaa. Huduma zote hizi ni msingi mzuri wa kuimarisha afya za wananchi na kuepuka kutumia gharama kubwa kutibu wananchi kwa mambo yanayoepukika kupitia utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anaunga mkono mpango wa kuwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii kutokana na umuhimu wao kwani wana mchango mkubwa katika sekta ya afya na wamesaidia sana kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya, kupunguza mzigo kwenye vituo vya afya kwa kuimarisha kinga ya maradhi katika jamii.

"Ukiangalia ugonjwa wa kifua kikuu, katika kila wagonjwa 100, wagonjwa 50 wameibuliwa na watoa huduma wa afya ngazi ya jamii, kwa hiyo watakwenda kupunguza gharama za kuwatibu watu. Taasisi ya Saratani ya Ocean Road wagonjwa wanafikia tatizo likiwa hatua za mwisho, kisukari na matatizo ya figo wagonjwa wanachelewa kubaini matatizo haya," amesema Ummy akimaanisha kupitia wahudumu hao wa afya katika ngazi ya jamii watasaidia sana kuwaibua mapema wale wenye matatizo hayo kungali mapema.

Kiukweli Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hasssan akisaidiwa na wataalamu wa Wizara ya Afya inaonekana imejizatiti kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi kwa kuhakikisha inafanikisha mahitaji yote muhimu yanayohitajika kwa watoa huduma hawa yakiwemo masuala ya mafunzo kwa miezi sita darasani na nje ya darasa na vitendea kazi.

Kwa watakaofanikiwa kuchaguliwa na hatimaye kuhitimu mafunzo, watakuwa na jukumu la kufikia kaya 25 kwa wiki na kaya 100 kwa mwezi huku wakitakiwa kutoa ripoti kwenye uongozi wa kituo cha afya kilichopo karibu nao chini ya mtendaji wa kata.

Aprili 06, 2024, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (Tamisemi) ilitangaza nafasi za kazi kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii 8,900 watakaokwenda kutekeleza afua jumuishi za afya, lishe na ustawi wa jamii katika ngazi za vitongoji na vijiji.

Katika tangazo hilo, awamu ya kwanza ya mpango huo utaanza kwenye mikoa 10 na halmashauri mbili kwa kila mkoa na itakayonufaika ni Geita wahudumu 920, Kagera 878, Kigoma 1,094, Lindi 1,724, Mbeya 836, Njombe 746, Pwani 480, Songwe 774, Tabora 966 na Tanga 482. Bada ya kukamilika awamu hii ya kwanza, utekelezaji wa mpango huu utaendelea kwenye mikoa na halmashauri zingine za Tanzania Bara.

Wahudumu wa afya ngazi ya jamii watasambazwa kwenye kila kitongoji au mtaa ambapo kwa kila mtaa au kitongoji kitapata wahudumu wawili yaani mwanaume na mwanamke.

Hivi karibuni, kwenye kikao kifupi baina ya mawaziri kutoka wizara za kisekta na ugeni kutoka nchini Uingereza ukiongozwa na Waziri wa Uingereza na Maendeleo ya Afya, Andrew Mitchel, Waziri Ummy aliendelea kusisitiza umuhimu wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

"Mikakati hii ambayo tumeanza nayo ya utoaji wa Elimu ya Lishe pamoja na Uzazi wa Mpango kwa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ili watumike kutoa elimu ya afya hizo kwa wananchi kwa kuwa wao ndio wapo karibu zaidi na wananchi," amesema Ummy.

Hivyo basi, wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni watu muhimu sana. Kwa muktadha huo wahakikishe wanatimiza majukumu yao ipasavyo ili kuendelea kulinda afya za wananchi.

Wahudumu hawa wajue wana deni katika udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza kama kifua kikuu na malaria na magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, pesha, saratani na kadhalika.

Pia tunawatarajia kusaidia katika kudhibiti magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, masuala ya afya ya uzazi, lishe, mama na mtoto na usafi wa mazingira.

Serikali, wizara na wananchi kwa ujumla tunawategemea wahudumu hawa wa afya ngazi ya jamii kuwa sehemu ya kuboresha afya za wananchi. Msituangushe tafadhali.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Unapita njia ipi kwenye maisha?

WENGI tumejengewa imani kuwa, maisha yanakuja yenyewe na ni kudra tu.


Tumeamini kuwa kila kinachotutokea, tumepangiwa au ni bahati. Dhana hii pamoja na kuwa ina ukweli, lakini imepokelewa na kutumika vibaya kwa jamii hususan za Ki-Afrika, wakidhani ndiyo majaliwa na hakuna namna nyingine.

Dhana hii imefanya watu kutopanga malengo na kuamua hatma zao. Jamii zilizoendelea walielewa kuwa, maisha yanapangwa na mhusika kuanzia kwenye aina ya taarifa (maarifa) anayoyapokea zaidi ambayo yanajenga mtazamo wake na kuathiri ukuaji wake.

Kila mtu ana uwezo ndani yake. Wewe unayesoma makala hii pia umezaliwa na uwezo mkubwa ndani yako, uwezo unaoweza kubadilisha maisha yako na ya wale wanaokuzunguka, uwezo unaoweza kuleta mabadiliko kwenye eneo lako la kazi, uwezo unaoweza kubadili hali yako ya kiuchumi na kimahusiano, huu ni ukweli ambao watu wengi hawaukubali au wanaukubali ila hawauamini. Lakini haitoshi tu kujua una uwezo ndani yako, unatakiwa uuendeleze huo uwezo ukitambua kuwa, ziko njia mbili ambazo wanapita watu wote.

Njia ya kwanza inaitwa "Njia kuelekea Ukuu" (the path to Greatness). Njia hii inakufanya wewe kuhusika kikamilifu kuibua na kutumia nguvu na uwezo ulionao. Mchakato huo ndiyo safari ya kuyabadili maisha yako na kutoa mchango wako kugusa na kuhudumia wengine. Njia hii hufuata mtiririko wa ukuaji unaoanzia ndani kuja nje Sequential growth - from inside-out). Mtiririko huu unaanza na wewe kuamua maeneo ambayo unataka kuwa bora, unachagua aina ya taarifa na maarifa yatakayokufikisha kwenye ubora unaoukusudia, tatu ni kujitoa kwa dhati kwa kupunguza mambo mengine ili kutoa muda wa kutosha kujipatia maarifa hayo mahsusi.

Mafanikio yote huanzia ndani yako, lakini kinachofanya ukuaji ndani yako ni aina ya taarifa na maarifa ambayo unayaruhusu kuingia ndani yako mara kwa mara. Njia hii ya kwanza inatengeneza nguvu ya ubunifu (Creative Forces) ndani yako kukuwezesha kuwajibika kufanya maamuzi ya kuzishinda changamoto zote zilizo ndani na nje yako. Kikubwa cha kufahamu ni kwamba, njia hii ni ile ambayo wewe unapanga na kuamua na kuweka bidii. Hii ndiyo yenye asilimia kubwa ya kufikisha kwenye ukuu.



Njia ya pili inaitwa Njia ya Kujifananisha (The path to Mediocrity).

Njia hii inauzima au kuua uwezo uliomo ndani yako, watu wengi bila ya kujua wanapita njia hii. Kwenye njia hii, uwezo na nguvu ndani yako hazihusiki kwenye ukuaji wako, unajikuta unaishi tu kulingana na mazingira yako, unaangalia tu wanaokuzungua wanafanyaje na hakuna chujio ndani yako. Lile eneo la maamuzi (Centre of decision and choices) ndani yako linakuwa halifanyi kazi. Kinachotokea ni kuathiriwa moja kwa moja na mambo ya nje nawe kuwa hivyohivyo mazingira ya nje yalivyo. Kwenye njia hii, maisha yanaamua na kukufanya kuwa mtu wa aina fulani (culture software) kwa maana ya kwamba, mfumo unaokutengeneza unakuwa nje ndani (outside-in),ambapo unajikuta unakuwa na mtindo wa kutafuta tu njia rahisi kuishi (short-cut au quick fix kwenye maisha).

> **Lakini kumbuka haitoshi kuutambua na kuuendeleza tu uwezo wako, unahitaji kujua namna ya kuutumia huo uwezo (know how to express your...**

Ni vyema kama utaamua kuifuata njia ya kwanza (The path to Greatness) sababu itakayoendeleza na kukuza nguvu na uwezo wako, itakutengeneza na kukujengea uwezo wa kutoa mchango wako duniani.

Lakini kumbuka haitoshi kuutambua na kuuendeleza tu uwezo wako, unahitaji kujua namna ya kuutumia huo uwezo (know how to express your potential) katika namna ambayo itagusa maisha yako na maisha ya watu wengine.


Mwandishi Stephen Convey katika kitabu "The 8th habit" amefundisha vizuri njia hii ya "the Path to Greatness", unaweza kutafuta kitabu chako ukasoma.

Kliniki ya Fikra inatambua na kumshukuru mchango mkubwa wa Mwalimu na Paul Masatu kwenye ujenzi wa makala hii. Yeye amejenga msingi wa maarifa haya leo. Mungu ambariki kwa mchango mkubwa.

Kama unapenda kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu au miongozo iliyotangulia, (Unaweza kuwa Taasisi Binafsi au ya Serikali, Kikundi cha kijamii, Kanisa, Umoja, NGO, Mtu binafsi n.k) karibu sana, tutashirikiana kwa neema na msaada wa Mungu.

Karibu tuwasiliane kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com na kwenye mitandao ya kijamii.

Paul Mng'ong'o



Na Hamisi Kibari

# ROHO NYEUSI

"NAIMA, Naima... we Naima," nilisikia sauti ya bibi aliyekuwa amelala kwenye kitanda kilichokuwa pembeni mwangu akiniita.

"Abee, bibi," niliitika. Nikamsabahi. Nikanyayuka na kuketi kitandani. Nilijua kumekucha, bibi ananiamsha ili tuswali Swala ya Alfajiri.

"Ninajisikia vibaya. Kichwa kinaniuma sana, moyo unanienda mbio. Hebu nipe dawa zangu kwenye kabati hapo ninywe," alisema.

Nikashuka kitandani, nikawasha taa na kumpa dawa zake za moyo kama alivyoniagiza. Kabla sijarudi kitandani baada ya kugundua ilikuwa bado usiku mnene, akaniambia nichukue kitambaa na maji ili nimfute mwilini kupunguza joto la homa.

Kwa kweli nilipomgusa, alikuwa na homa kali hadi nikashituka.

"Bibi, nikawaamshe majirani?" Nilimuuliza wakati nikiendelea kumfuta maji huku yeye akitetemeka na kugugumia kwa maumivu.

"Hapana, in shaa Allah, Mwenyezi Mungu Mtukufu atanisaidia hadi asubuhi halafu utanisindikiza hospitali. Nahisi nimepatwa na malaria kali. Nilianza kusikia hali tofauti tangu jioni. Nisomee Kuran na dua kwenye maji kisha unipe."

Nikamsomea. Akanywa yale maji na mengine akajipaka usoni. Nilimwacha akiendelea kugugumia maumivu, nikapitiwa na usingizi.

Niliposhituka kutoka usingizini, nikahisi kulikuwa kumekucha.

"Asalaamu alaikum," nilimtolea salamu bibi nikiamini atakuwa macho, lakini hakujibu salamu yangu.

"Ninakusalimu Binti Musendo, Asalaamu alaikum. Bado umelala?" Nikasema, safari hii kwa kupaza sauti zaidi. Lakini hakujibu salamu yangu. Nikahisi alikuwa bado usingizini kutokana na kuhangaika na ugonjwa uliompata usiku huo.

Mwanga wa nje kupitia kwenye nyufa za madirisha na milio ya ndege kwenye miti iliyo jirani na nyumba ya bibi vilinijulisha kwamba haiwezekani kwamba bado ni usiku. Nilihisi hata jua linakaribia kuchomoza.

Niliona ni vyema nimwamshe tuswali kisha nijiandae kwenda shule, kama bibi atasema ameamka vizuri au tufanye maandalizi ya kwenda hospitali. Ilikuwa haiwezekani bibi aamke na kisha kuswali peke yake bila kuniamsha, labda kama atajua nina dharura ya kisheria inayoniweka mbali na swala kwa sababu nilikuwa tayari nimevunja ungo.

Kutokana na bibi kuhangaika na kilichokuwa kinamsumbua usiku huo, nilihisi ilikuwa ndio sababu ya kuchelewa kuamka kutokana na kukaa muda mrefu akiwa macho.

Ni mara chache sana bibi ambaye tulikuwa tukilala pamoja chumbani mwake kupitiwa na usingizi wakati wa swala hadi kuchomoza jua. Siku za aina hiyo zinaweza kuhesabika.

Bibi yangu aliyekuwa akijishughulisha na biashara ya kuuza mbogamboga na nyanya katika soko kuu la mji wa Geita, hata kama yuko taabani kiasi gani, alikuwa hawezi kupitwa na kipindi

Bado bibi hakuamka. Nikahisi kuchanganyikiwa. Haikuwa hali ya kawaida. Kwa kuzingatia kwamba nyumba nzima tulikuwa peke yetu, mimi na yeye, nikapata wazo la kuwaamsha majirani. Mjomba ambaye ni mtu wa kuja na kuondoka, hakuwepo nyumbani

"Kwa hiyo unataka nini, Mtoto wa Boksi?" mke wa Mzee Lukanya ambaye alikuwa amesogea jirani zaidi, akahoji na hasa aliposoma uso wangu ambao ulionesha mashaka makubwa. Yeye ni kati ya watu walioendelea kuniita jina langu la utotoni la Mtoto wa Boksi.

karibu yao nikiwaangalia majirani zetu hao ambao sasa walikuwa wakionekana vizuri baada ya mwanga wa nje kuongezeka.

Nilizidi kuogopa kwa kitendo chao cha kuangaliana huku mke wa mwalimu akiendelea kutikisa kichwa.



cha swala. Ataswali kwa namna yoyote, akiwa amekaa ama amelala kitandani.

Nilishuka kitandani, nikasogea kitandani mwake. "Bibi, bibi... Amka. Kumeshakucha. Swalaa."

Bibi yangu, maarufu kwa jina la Binti Musendo ingawa jina lake halisi ni Kauthar Musendo, hakujibu kitu. Hali iliyonifanya nishawishike kumtikisa. Bado niliamini kwamba kutokana na kuhangaika usiku ndio maana alilala fofofo namna ile.

"Bibi, bibi... amka...". Hakuitika wala kujitikisa. Ghafla nilihisi moyo ukinienda mbio kwani haikuwa kawaida kumwamsha bibi hadi kumtikisa kiasi kile bila kushituka kutoka usingizini.

Nilifungua dirisha na nuru kidogo iliingia chumbani, lakini ilikuwa si ya kuniwezesha kumwona usoni sawasawa. Nikawasha taa. Mpaka sasa sijui kwa nini nilitaka nimwone usoni.

Nilimwona amefumba macho nikaamini bado ana usingizi mzito. Nikamtikisa, sasa kwa nguvu zaidi kama ambavyo yeye amekuwa akifanya anaponiamsha, hasa siku ambazo ninachelewa kulala kwa ajili ya kujisomea.

baada ya kupata kibarua kwenye machimbo ya dhahabu wilaya jirani ya Mbogwe.

Nikatoka hadi nyumba ya jirani yetu ambako nilimkuta Mzee Hashim Lukanya, mwalimu mstaafu, akifagia uwanja wa nyumba yake asubuhi hiyo.

"Mwalimu... Bibi sijui kawaje... Namwamsha, namwita wala hajibu kitu. Niko mwenyewe tu nyumbani," nilisema huku nikitetemeka kwa ndani baada ya kumtolea salamu. Licha kustaafu, bado tuliendelea kumwita mwalimu. Si mimi peke yangu bali jamii nzima.

"Unasemaje?" Alinihoji akisimama kufagia. Wakati huo mkewe ambaye alikuwa akitoa nguo nje kwa ajili ya kufua akawa anasogea jirani yetu.

"Ninamwamsha bibi haamki... Hadi nimemtikisa sana lakini wapi... Nyumbani niko peke yangu," nikarudia kusema.

"Mh! Labda kalala tu. Usiwe na wasiwasi Naima... Kwani mjomba wako toka aende kwenye migodi hajarudi? Juzi niliona mtu kama yeye hapo nyumbani?"

"Hajarudi."

"Ninamwamsha bibi lakini haamki. Nimeshamtikisa mara kadhaa lakini wapi... Mimi amenishangaza. Ninaomba mkamwangalie."

"Baba Amina, yaani hali kama anayosema Mtoto wa Boksi unaichukulia masihara. Twende tukamwangalie," akashauri mwanamke huyo.

Baada ya sekunde kadhaa, mimi, Mwalimu Lukanya na mkewe tulikuwa chumbani kwa bibi. Majirani zetu hao ambao ndio wa karibu zaidi walianza kwa kumwita bibi lakini hakuitika hata walipozidisha sauti.

Mke wa Lukanya alimtikisa lakini hakuonesha kushituka. Akapeleka mkono wake kwenye kifua cha bibi pale kitandani na kusikiliza mapigo. Akainuka na kumwangalia mumewe huku akitikisa kichwa.

Mwalimu Lukanya yeye alipeleka kidole chake kwenye pua za bibi na kusikilizia kisha akaangaliana na mkewe.

Muda wote mimi ambaye karibu maisha yangu yote hadi wakati huo nilikuwa nikiishi na bibi kiasi cha awali kudhani ndiye mama yangu mzazi, nilikuwa nimesimama

Mwalimu Lukanya alinishika mkono, tukatoka naye nje huku akimwacha mkewe akiwa bado ameduwaa pale pembeni mwa kitanda cha bibi.

"Una namba ya simu ya mjomba wako?" Aliniuliza baada ya kuvuka kizingiti cha mlango akiwa bado amenishika mkono.

"Mjomba siku hizi hana simu... Kwani mmegundua nini?" niliuliza kwa wahaka. Moyo ulizidi kunienda mbio kwani pamoja na udogo wangu, nilihisi kuna kitu hakiko sawa.

"Mama yako mzazi, Subira, una namba yake ya simu?" Mwalimu aliniuliza.

"Namba ya mama sina. Hata bibi hana. Yaani mama hana kabisa mawasiliano na mtu," nilisema na kuongeza kwamba namba niliyo nayo ni ya mama mdogo aliyekuwa masomoni.

Mzee Lukanya aliendelea kutafakari wakati mkewe pia akitoka nje, mimi nikamgeukia tena. "Kwani Mwalimu, bibi kapatwa na nini?"

"Lete namba ya mama yako mdogo," Mwalimu alisema.

***Itaendelea***

# Idara dhidi ya ufisadi Nigeria yapata Dola mil. 25 zilizoibwa

**ABUJA, Nigeria**

IDARA ya Kupambana na Ufisadi nchini Nigeria, imesema kuwa tayari imepata karibu Dola milioni 27 kufuatia uchunguzi dhidi ya Waziri wa serikali aliyesimamishwa kazi pamoja na maafisa wengine.

Rais Bola Tinubu, alimsimamisha kazi Waziri wa Masuala ya Kibinadamu na Kuangamiza Umaskini, Betta Edu, Januari, mwaka huu, kufuatia tuhuma kwamba alielekeza fedha za umma kwenye akaunti binafsi za benki.

Rais Tinubu pia alimsimamisha kazi Kiongozi wa Uwekezaji wa Jamii kwenye wizara hiyo, Halima Shehu, kutokana na tuhuma za ufisadi.

Kwa mijibu wa Shirika la Habari la Reuters, Shehu alikamatwa na kisha kuachiliwa kwa dhamana.

Taarifa zaidi zinasema kuwa aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Kupambana na Umaskini, Sadiya Umar Farouq, pia alikamatwa ili kusaidia kwenye uchunguzi.

Rais Tinubu tangu kuchukua madaraka mwaka jana, amefanya marekebisho kadhaa ya kiuchumi, wakati pia akiwasimamisha kazi maafisa kadhaa serikalini, akiwemo Gavana wa Benki Kuu, Godwin Emefiele. VOA.

**Rais Tinubu pia alimsimamisha kazi Kiongozi wa Uwekezaji wa Jamii kwenye wizara hiyo, Halima Shehu, kutokana na tuhuma za ufisadi.**



Rais Bola Tinubu

# Mapigano yazuka katika mpaka Tigray, Amhara

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

MAPIGANO yamepamba moto katika moja ya maeneo yanayozozaniwa kati ya Majimbo ya Tigray na Amhara nchini Ethiopia katika kipindi nadra cha vurugu baada ya makubaliano ya amani yaliyotiwa saini mwishoni mwa mwaka 2022 kumaliza moja ya vita mbaya zaidi barani Afrika.

Wilaya ya Raya Alamata inayozozaniwa na majimbo yote mawili,ilikuwa chini ya Tigray Kusini kabla ya vita kuanza, lakini tangu wakati huo, imekuwa chini ya udhibiti wa vikosi vya Amhara.

Wakazi waliambia BBC kwamba mapigano yalianza wikendi na kuendelea kwa siku kadhaa.

Maafisa wa Amhara waliwashutumu wapiganaji wa kundi la Tigray Peoples Liberation Front (TPLF) kwa kuanzisha mashambulizi huku Mkuu wa eneo la Kusini mwa Tigray, akisema wanamgambo wa Amhara walifyatua risasi.

Chama cha upinzani cha National Movement of the Amhara (NaMA) katika taarifa yake, kililaumu TPLF ambayo ilisema ilikuwa ikianzisha uvamizi.

Akiandika kwenye X, Getachew Reda, Mkuu wa Utawala wa muda wa Tigray, alisema maendeleo ya hivi karibuni katika maeneo hayo hayakuhusisha migogoro kati ya vikosi vya Tigray na Serikali ya Shirikisho au kati ya mikoa jirani ya Tigray na Amhara.



Alilaumu maadui wa mpango wa amani kutoka karibu au mbali kwa matukio bila kutaja wao ni nani.

Haijabainika kama kuna majeruhi wowote, lakini vyombo vya habari vinavyounga mkono Amhara, viliripoti kwamba vikosi vya Tigray viliingia katika baadhi ya wilaya siku ya Jumatatu.

Hivi majuzi Serikali ya Shirikisho imesema Jeshi litadhibiti maeneo yenye migogoro hadi suluhu litakapotolewa.

Kuna wasiwasi kwamba hii inaweza kuzidisha mzozo unaoendelea tangu Agosti, mwaka jana katika eneo la Amhara, Ethiopia lenye watu wengi zaid kati ya wanamgambo wa ndani na Jeshi. VOA.

# Baraza la Mawaziri lakutana kujadili jibu shambulio la Iran

**YERUSALEM, Israel**

BARAZA la Mawaziri la Vita la Israel, limekutana kujadili jibu lake kwa mashambulizi ya Iran yasiyo na kifani.

Hata hivyo, Israel haikuweka hadharani iwapo uamuzi ulikuwa umefikiwa.

Washirika wake wamelaani vikali vitendo vya Iran, lakini wameitaka Serikali ya Benjamin Netanyahu, kujizuia.

Wakati Iran ikiashiria kwamba inazingatia suala hilo kumalizwa, Mkuu wa Jeshi la Israel alisema shambulio hilo halitakosa jibu.

"Tunatathmini hatua zetu dhidi ya shambulio hili la makombora mengi, makombora ya kusafiri, UAV hadi eneo la taifa la Israel litajibiwa," Luteni Jenerali Herzi Halevi, alisema lakini hakutaja hatua itakayochukuliwa au kutoa mpangilio wa nyakati.



Benjamin Netanyahu

Mkuu wa zamani wa CIA, David Petraeus, alikiambia kipindi cha World Tonight cha BBC Radio 4 kwamba, Washington haitaki kuhatarisha ustawi wa uchumi wa dunia kutokana na Israel kulipiza kisasi dhidi ya Iran.

Jenerali Petraeus, ambaye pia aliviongoza vikosi vya kimataifa vya Iraq na Afghanistan, alisema shambulio la Iran lilikuwa jambo kubwa san na kwamba nchi za Magharibi zilipaswa kuelewa jinsi hii ilikuwa muhimu kwa Israel.BBC.

# Wafadhili wa dunia waahidi Doa bil. 2.1 kukabili gogoro la kibinadamu Sudan

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amesema wafadhili wa dunia, wameahidi Dola bilioni 2.1 kusaidia kukabiliana na mgogoro wa kibinadamu nchini Sudan iliyoharibiwa na vita.

Rais Macron alikuwa akizungumza jijini Paris juzi Jumatatu mwishoni mwa mkutano wa kimataifa uliopitishwa kuhamasisha kuhusu umuhimu wa msaada wa kifedha kwa juhudi ambazo ufadhili umepungua kwa kiasi kikubwa.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, aliitaka dunia kutosahau kuhusu watu wa Sudan, huku akitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano katika maadhimisho ya mwaka mmoja wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya taifa hilo la Barani Afrika.

"Ni vita dhidi ya maelfu ya raia ambao wameuawa na dazani za maelfu ya watu waliojeruhiwa," Guterres aliwaambia waandishi wa habari katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa huko New York na kuongeza:

"Ni vita dhidi ya watu milioni 18 wanaokabiliwa na njaa kali na jamii sasa zinatazama tishio la njaa katika miezi ijayo."

Mapigano yalizuka katika Mji Mkuu wa Sudan, Khartoum, mwaka mmoja uliopita kati ya Majenerali wapinzani, mmoja akiongoza Kikosi cha Wanajeshi wa Sudan (SAF) na mwingine Kikosi cha RSF. Uadui ulienea haraka nchi nzima.



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron

UN inasema zaidi ya watu milioni nane wamekimbia makwao kutafuta usalama na milioni 1.8 kati yao wamehamia nchi jirani.

Jitihada za kuwasaidia mamilioni ya watu wanaokabiliwa na njaa kutokana na vita, zimezuiliwa na kuendelea kwa mapigano yanayoendelea na vikwazo vilivyowekwa na pande zinazopigana.

Aidha, pia imeathiriwa na ukosefu wa ufadhili wa kutosha kutoka kwa Jumuiya ya Kimataifa kutokana na mataifa mbalimbali kuhitajika kufadhili migogoro mingine ya kimataif, ikiwa ni pamoja na Gaza na Ukraine.VOA.

# Magori awataka Wana-Simba watulie

## ●Asema hakuna safari isiyokuwa na mabonde na miinuko!

**Na Mwandishi Wetu**



MSHAURI wa masuala ya soka wa Rais wa Heshima wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori amewataka wanachama na mashabiki wa Wekundu hao wa Msimbazi watulie katika kipindi hiki timu yao inapitia wakati mgumu.

Magori amewashangaa Wanasimba kuingia katika mtego wa kuibeza timu yao wakati haijafanya vibaya kama inavyovumishwa na wapinzani wao wasioitakia mema timu yao.

Kiongozi huyo aliyekuwa CEO wa kwanza baada ya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa klabu ya Simba, amefafanua kwamba mbali ya Simba kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika sambamba na kutupwa nje katika michuano ya

Kombe la Shirikisho la CRDB, bado klabu yao ndiyo yenye

mafanikio kuliko timu yoyote Tanzania kwenye kipindi cha miaka sita sasa.

"Safari ya Simba mpya ilianza mwaka 2018, safari ambayo mpaka sasa haijakamilika! Mategemeo ya kila Mwana-Simba ni kuwa baada ya mabadiliko ya Katiba ya Januari mwaka huu 2024, Serikali itakamilisha mchakato huo hivi karibuni ili mfumo uanze kutekelezwa barabara," amedai Magori.

Magori ambaye amewahi kuwa Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), ametanabahisha kuwa, katika kipindi hiki cha miaka sita ya Simba mpya, timu yao imepiga hatua kubwa kimaendeleo tafauti inavyobezwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari na mitandaoni na Wanasimba kuingia mkenge wa kutukana wachezaji na viongozi wao.

Ameeleza kuwa, Simba imetoka katika timu isiyojulikana ni ya ngapi Afrika (unranked) mpaka namba 5 Afrika, imetoka kwenye bajeti ya shilingi bilioni 3 mpaka bajeti ya zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa mwaka, timu yao imechukua ubingwa wa Tanzania mara nne mfululizo sambamba na kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho(FA) mara 3 mfululizo na kuhoji inakuajje timu mbovu?





> "
> **Ameyataja mafanikio mengine ya Simba ndani ya miaka sita kuwa ni pamoja na kutwaa Ngao ya jamii mara 4, kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mara 4, kufika robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Afrika mara moja, msimu huu imekuwa miongoni mwa timu nane**

Ameyataja mafanikio mengine ya Simba ndani ya miaka sita kuwa ni pamoja na kutwaa Ngao ya jamii mara 4, kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mara 4, kufika robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Afrika mara moja, msimu huu imekuwa miongoni mwa timu nane Afrika zilizoshiriki mashindano mapya ya Ligi ya Soka Afrika (Football League).

Katika kipindi hicho cha miaka sita Magori ameyataja mafanikio mengine ya Simba ni kujenga viwanja vyake vya mazoezi, timu yao ya wanawake, Simba Queens kuchukua ubingwa wa Tanzania mara 3 sambamba na timu hiyo kufika nusu fainali ya Ligi ya Wanawake Afrika mwa juzi.

"Mafanikio haya katika kipindi cha miaka 6 siyo madogo kwa namna yoyote ile! Hakuna Timu yoyote Tanzania iliyowahi kufikia mafanikio haya!" Amejinasibu Magori.

Badala ya kuwalaumu viongozi wao Magori amewataka Wanasimba wenzake kutoa pongezi kuanzia kwa Mwekezaji wao Mohamed Dewji 'Mo', Bodi ya Simba na Menejimenti ya Klabu hiyo, walimu na wachezaji!

"Nafahamu hamu ya Wanasimba ni kurudisha Ufalme wetu hapa nyumbani na kuvuka hatua ya robo fainali kwenye michuano ya CAF! Ndoto hizi haziwezi kufikiwa kwa mabishano, mvurugano na ugomvi bali kwa kukaa chini na kujipanga kimkakati!" Amesihi Magori.

Pia kiongozi huyo mwandamizi amewataka Wanasimba kupuuza uvumi unaodai kwamba Mwekezaji wa 'Mo' amejiweka kando na klabu hiyo kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa mabadiliko ndani ya klabu hiyo.

"Naomba niwahakikishie baada ya mazungumzo na Rais wa Heshima wa Klabu Mohamed Dewji amekanusha uvumi huo, naomba niwatoe hofu kuwa Mo hajawahi kuiacha Simba na hataiacha Simba na ataendelea kushirikiana na uongozi katika kujipanga upya kurudisha heshima ya Simba na kuzidi kuimarika!" Ameeleza Magori huku awasisitiza Wana - Simba kuachana kelele za mitandaoni, wawe nyuma ya timu yao kwani Simba imara inakuja!

# TOT ni bandika bandua Tamasha la Dk. Samia

## ● Yajifua vilivyo kuhanikiza vibao vipya TTCL Kijitonyama
## ● Mrisho Mpoto, Msechu, Msagasumu, Barnabas kutoa 'kampani'

**Na Hamid Yassin**

KUNDI la Tanzania One Theatre (TOT) linalomilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) wanajifua kwa wiki ya pili sasa kwa ajili ya Tamasha maalumu Jumamosi la kuenzi kazi zilizotukuka zilizofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika miaka yake mitatu ya uongozi wa taifa hili.


Gazeti hili la Uelekeo limekuwa likihudhuria mazoezi hayo yanayofanyika kwenye ukumbi wao wa nyumbani wa CCM Mwinjuma Mwananyamala na kushuhudia kazi pevu ya kuandaa na kufanyia mazoezi ya nyimbo kadhaa mpya zitakazosikika kwa mara ya kwanza kwenye Tamasha hilo.

TOT ambayo sasa ipo chini ya uongozi wa msanii maarufu wa muziki wa taarabu Malikia Khadija Omar Abdallah Kopa imesema kundi lao lilianzishwa mwaka 1992 kwa kazi maalumu ya kupigia 'chapuo' Chama tawala CCM na Serikali hivyo sasa wanachukua jukumu lao la kuzifikisha kwa wananchi kazi hizo alizofanya Rais Dk. Samia kwa njia ya sanaa kama kawaida yao.

Katibu Mipango wa TOT, Omari Mussa Jenela almaarufu kama Bokilo ameliambia Uelekeo kuwa, uzinduzi wa nyimbo hizo utakaofanyika kwenye Viwanja vya TTCL Kijitonyama utakuwa na nyimbo sita mpya toka fani zao za kwanya, taarabu na muziki wa dansi.

Bokilo amezitaja nyimbo hizo kuwa ni pamoja na 'Jicho la Mama' na 'Dk. Samia Mwamba' ambazo ni za dansi huku upande wa kwaya wanakuja na nyimbo za 'Kanyaga twende' na 'Twende kwa pamoja' zilizotungwa na mwimbaji wa kundi hilo, Meka Twalib huku kibao cha tatu kinachokwenda kwa jina la 'Kazi iendelee' kimetungwa na msanii mwingine wa kundi hilo, Peter Kakondeli.

Katibu Mipango huyo ambaye pia ni kiongozi wa shoo wa TOT, amepasha kuwa, kutakuwa na wimbo maalumu wa Chama uliotungwana Omari Ally, lakini wanahifadhi jina lake hili kuwashtukiza mashabiki wao pale TTCL Kijitonyama.







Mbali na nyimbo hizo za dansi na kwaya za kumuenzi Dk. Samia, pia Bokilo amesema kutakuwa na burudani ya nyimbo za mipasho, yaani taarab ambapo watakaohudhuria Tamasha hilo, watapata fursa ya kusikia vibao vipya vinne maridhawa sambamba na nyimbo zote za zamani za dansi, kwaya na taarab za kundi hilo.

"Hatutawaacha hivi hivi watakaohudhuria, tutawapigia hadi nyimbo zetu za zamani kama vile 'Mtaji wa Maskini,', 'Aminata', 'Mtu Pesa', 'Walimwengu', 'Kisa cha Mpemba', 'Jirani' na nyingine kadhaa," amesema Bokilo.

Kwa upande wa taarabu utakaoongozwa na Malikia Khadija Kopa tayari umekamilisha kufanyia mazoezi vibao vinne vya 'mipasho' ambayo kwa ubora wake lazima vitapagawisha watu pale TTCL Kijitonyama.

Kopa aliyeibukia kundi la taarabu la Culture la Zanzibar kupitia nyimbo za 'Kadandie', 'Nimejisilimu', 'Wa hoi' na 'Daktari'; kabla aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TOT, marehemu John Komba kumvuta kundi hilo mwaka 1992 mara baada ya kuasisiwa kwake, amewataka mashabiki zake kutokosa burudani hiyo Jumamosi.

Ameweka mambo hadharani kwamba kabla ya kuporomosha hivyo vibao vipya, ataanza na bashirafu ya mipasho yake ya zamani iliyotikisa Afrika Mashariki na Kati ya 'Ngwinji, 'Mambo iko huku', 'TX Mpenzi', 'Kishata mtaa', 'Mwanamke Mambo', 'Una moyo', 'Full Stop', 'Nalijua Jiji', 'Mjini Chuo Kikuu', 'Top in Town', 'Wrong Number' na nyinginezo za kutosha.

Wakati huo huo, Siku hiyo ya Jumamosi TOT watapewa 'kampani' na wasanii kadhaa wa muziki wa Bongo Fleva wataongozwa na Peter Msechu na Elias Barnaba Inyasi, upande Singeli Msaga Sumu atashuka na vibao vyake vya 'Mwanaume Mashine', 'Unanitega shemeji' na nyinginezo zinazotmba hivi sasa.

Mwanamuziki nguli wa kughani mashairi hapa nchini, Mjomba Mrisho Mpoto pia atakuwepo kwenye Tamasha hilo la Dk. Samia na ameahidi atashuka na nyimbo kadhaa ikiwemo maalumu itakayoelezea yote yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais hususani lile la kupigania kuwatua wakina mama ndoo za maji.



# Ras Nganyagwa katika mabonde na milima ya muziki-2

***Wiki iliyopita tuliona simuliza ya mwanamuziki mkongwe wa Reggae. Innocent Nganyagwa akisimulia jinsi alivyojitosa katika muziki na kupitia 'msoto' mkubwa. Endelea kupata simulizi hii sehemu ya pili ya kusisimua kupitia gazeti lako hili pendwa la Uelekeo.***



**Ras Innocent Nganyagwa akipokea tuzo wa wimbo bora wa Gila toka kwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete wakati huo akiwa Waziri wa Uhusiano wa Kimataifa na Mambo ya Nje.**

NILIKATAA kukata nywele ila walishindwa kunifukuza maana mchango wangu ulikuwa adhimu sana kwenye Bendi. Nikaunda Bendi ya kwangu mwenyewe 'The Inspirational Sounds' wanamuziki wangu hawakunielewa wakaacha bendi nilipokuja Dar es Salaam Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kufanya usajili.

Nikaamua kurudi jijini na kuwa 'Solo Artist' tukaandaa Tamasha kubwa la Reggae kwa kushirikiana na Enrico Figuieredo, Pompydou Dominick na Issack Waziri nuru ikaangazika nikapata Promo magazetini. Nikaitwa kujiunga na Bendi ya Makondeko Six Luguruni Mbezi, nikatumikia kwa uadilifu na kudunduliza mishahara hata nikafanikiwa kupata fedha za kurekodi albamu ya Money-Pesa (Life Controversies).

Baadaye pale Makondeko ndipo alipokuja marehemu Harila Yusuph Tongolanga (R.I.P) tukasugua sana mipini ya rhumba za Kimakonde kwa mtindo wa 'Ntavala' mimi nilikuwa mpiga besi mwenye mbwembwe nyingi za kucheza jukwaani, hata wakanipa a.k.a ya 'Kata Miwa' kwenye nyimbo za bendi hiyo 'Kila Munu avena kwao sehemu ya II', 'Tuvamu', 'Chipaleta', 'Mija Masudi' n.k.

Tongolanga alipenda sana kunihanikiza "Bomba Inno... bombaa....Inno...," wakati huo sijaanza kuitwa Ras Inno hata kule Iringa nilijipa a.k.a za 'Kaya Man' baadaye 'Man from the Hills' & 'Inno Ricky'.

Hatimaye baada ya kutoa Albamu yangu ya kwanza 'Money-Pesa' mwaka 1994 a.k.a ya Ras Inno iliyoasisiwa na aliyekuwa Mwandishi wa Gazeti la Mfanyakazi Ibrahim Hassan ikashika kasi. 'Gila' ngoma kutoka albamu hiyo ikahanikiza sana hatimaye ndoto zikaanza kutimia, nikakubalika katika medani ya tasnia na kukwea majukwaa mbalimbali kutumbuiza kama.

### VITONGOJI NA JAMAA WALIONISHIKA MKONO KIUHAKIKA

(Munisandesa- 'Muziki Ni Safari Ndefu Sana' inaendelea!

Katika kuhangaika kwangu kufikia malengo ya ndoto zangu kimuziki kuna vitongoji, jamaa na maeneo ambayo hayasahauliki kwangu kutokana na kunishika mkono kiukweli.

Nilipogomewa tungo zangu za reggae katika Bendi ya VICO Kanisani Katoliki Mshindo huku Bendi yangu Inspirational Sounds niliyoiasisi hatukuwa na vifaa toshelezo hivyo kuna wakati tulidoea vyombo vya VICO kinyemela lakini nikabainika, nikazuiwa.

Wapiga 'Solo' na 'Rythm' wangu Yusuph na Joseph Limba walikuwa wanasali Kanisa la Lutheran Mkabala na Soko Kuu pale Iringa Mjini, tukakimbilia kule tukawa tunafanya mazoezi kwa siri.

Lakini siku moja Mchungaji alisikia mirindimo tofauti na nyimbo za Kanisa alizozoea kusikia, akaamua kuja tulipokuwa, nasi tulipomuona kwa mbali anaelekea tulipo tulibadilisha gia na kupiga 'Gospo' alipotuuliza tulimwambia tulikuwa tuna-testi vyombo kwanza na alipotoka tu nje ya geti tukaendelea kungurumisha Ma-Reggae kama kawaida.

Awali mwanzoni kabisa nikiwa darasa la IV nilitunga wimbo wangu wa kwanza kabisa (Haukuwa katika miondoko ya Reggae), mazoezi ya utotoni tulikuwa tunafanyia nyumbani kwa Mzee Raidan Mtavangu aliyekuwa jamaa wa karibu na Baba yangu (Mzee Richard Nganyagwa), miongoni mwa marafiki zangu kati ya watoto wa Mzee Mtavangu ni Oscar Mtavangu tukiwa Kitongojini cha Keko Juu, Miburani, Temeke hapa jijini nakumbuka hamasa ilinigubika tulipoambiwa tutengeneze zana za sanaa shuleni (Kibasila Primary) nilitengeneza gitaa kwa galatoni la mafuta ya Okey yaliyokuwa maarufu sana wakati huo.

Miaka ya baadaye katika kuitafuta njia tulikuwa tunafanya mazoezi ya kukopi nyimbo za Bob Marley kwa kuimba tulipozipiga kwenye Santuri pamoja na rafiki yangu Taji Liundi (Master T) ambaye kwa sasa ni Mshehereshaji maarufu, tukatokota.

Taji akabwaga manyanga mimi sikukubali na ndipo baadaye nikakutana na kumfahamu Braza Richard Ndunguru a.k.a 'Khaki Man' ambaye alikuwa akipita mtaani kwetu (siku hizi mtaa huo unaitwa Mtaa wa Pume kutokana na Mkazi wa kwanza wa mtaa huo Mzee Salum Pume ambaye Mwanaye Idd Pume rafiki yangu wa utotoni ndiye Mjumbe wetu wa Mtaa kwa sasa).

Bro Rich alikuwa amefuga 'Vishungi' (Dreadlocks) na alivalia tofauti (Ki-culture) na hata mwendo wake ulijionesha kujiamini akiwa amebeba gitaa.

Siku moja nikamsimamisha na kumsabahi na kumuomba anifundishe kupiga gitaa aliniuliza kama nasoma nilimueleza kuwa nilishamaliza shule, alikubali na kuanza kunifundisha gitaa la rythm lakini mkono ulikuwa mzito kidogo akanihamishia kwenye gitaa la besi na baadaye nikawa mpiga drums.

Alipoasisi Bendi ya 'The Wailing Peasant' miongoni mwa tuliojiunga pamoja ni rafiki yangu Dennis Sakaya lakini yeye alibwaga manyanga mipini ilimshinda.

Bendi ya Peasant ilijinasibisha na Viwawa Kanisa Katoliki Parokia ya Mt. Maurus Kurasini kwa kuwa Khaki Man nami tulisali huko, Kitongojini kwetu yeye alikuwa kiongozi wa Kikundi cha Rozari mimi Makamu wake tukifanya Novena mfululizo nyumba kwa nyumba miaka ambayo hakukuwa na Jumuiya bado.

Bendi ilipofeli kiuchumi nilienda Iringa nikiwa na barua ya utambulisho ya Mt. Maurus nikajiunga na kikundi cha uimbaji cha Kanisa la Kigango cha Ndiuka ambako awali nilishaishi nilipoenda kumaliza elimu ya msingi huko ambapo baba yangu alikuwa Diwani wa Kata ya Ruaha.

Siku hizi ni Kata ya Igumbiro kutokana na ugatuzi wa mamlaka. Kigangoni hakukuwa na vyombo vya muziki nikaona kipaji kitafeli nikaomba barua nyingine zikawa mbili nikawasilisha VICO nikapokelewa kwa kuwa masharti ya Kanisa niliyatimiza tangu nilikotoka (Mt. Maurus na Ndiuka) ingawa baadaye nilitoka bendi hiyo kwa misukosuko niliyokumbana nayo na pia bendi yangu (Inspirational Sounds) ilivunjika.

Kitongojini Ndiuka ndipo nilipoitwa 'Mnyalukwale' (Kichaa) kwa maneno ya wasioelewa nilichokuwa nakitafuta ambayo yalimfikia Mzee wangu naye hakunielewa hasa wakati huo nilipoanza kufuga vishungi na kuwa mhafidhina mzingatia kanuni, nilipojaribu na wenzangu kuasisi tawi letu la kuabudia Urastafari la Ethiopian Orthodox juhudi ambazo hazikufanikiwa kutokana na wenzangu kuhama mkoa.



**Ras Innocent Nganyagwa na tuzo yake**

Moja kati ya upinzani wa baba kwangu nilipokataa kula nyama kwa misingi yangu mipya niliyoikumbatia na ili anishawishi, kila wikiendi akawa ananunua kilo tano za nyama ya ng'ombe na kilo tatu za kitimoto, ilihali tulikuwa tunaishi watatu tu nyumbani hapo yaani yeye Baba, mimi na Binamu yangu Jeniffer Mpunza (Anaishi Nairobi kwa sasa).

Nilipoona mambo yanakuwa magumu niliamua kurudi D'Salaam na kuwa mwanamuziki huru (Solo Artist) kama nilivyoeleza awali katika sehemu ya Pili ya simulizi hii.

Jamaa na Marafiki zangu walewale wa awali (Dennis, Taji, Braza Ndunguru na Issa Maguha) nilioanza nao ambao wengine waliachana na mipini mimi nikaendelea nd'o walionishika mkono kila nilipokutana na changamoto kwa sababu tu ya kupigania kipaji changu.

Hata nilipofanikiwa kurekodi na kurudi tena Iringa safari hii walioniita 'Mnyalukwale' walihofia hata kunisalimia hususan baada ya video nilizoshutiwa na Karim Sadrus wa Top Shop kutoka na nyimbo kuhanikiza kwenye Redio ya Taifa (RTD).

Baba yangu akageuka shabiki wangu namba mbili (Shabiki wangu namba moja ndani ya familia alikuwa hayati kaka Mathias, (nitamuelezea baadaye kwenye sehemu zinazofuata za simulizi).

Mzee wangu akitembea na kaseti yenye nyimbo zangu kwenye koti lake na kuwaonesha marafiki zake na Wana-Ndiuka akiwananga kwamba; "Mwanangu mliyekuwa mnamwita Mnyalukwale kumbe alikuwa anatafuta njia ya kutokea hapa alipofikia!"


Sadrus ni mtu aliyesababisha nifahamike kwa video za nyimbo zangu 'Gila', 'Watoto wa Mitaani' na 'Children On The Street' alizonishuti kutoka albamu yangu ya kwanza ya 'Money-Pesa' na kuzijumuisha katika 'Collection' ya video iliyosheheni nyimbo za wanamuziki wakubwa akina Kasaloo Kyanga na Kyanga Songa, Kalala Mbwembwe na King Kikii wachache miongoni mwa wengi waliokuwemo.

Albamu yangu ya 'Money-Pesa' ya mwaka 1994 ambayo majaribio mawili ya awali ya kuirekodi yaligonga mwamba hadi jaribio la tatu lililofaulu kwa fedha za kudunduliza za mshahara wa upigaji besi nilipokuwa naitumikia Bendi ya Makondeko iliyomilikiwa na marehemu Dk. Alex Khalid ambayo makao yake yalikuwa Makondeko Village Mbezi Luguruni mkabala na nyumbani kwa wazazi wa John Momadi aliyewahi kuwa Meneja wa Samuel Mreteni 'Jah' Kimbute.

**Itaendelea wiki ijayo.**

# Wachezaji bora wa muda wote NBA

Na Valensi Mbaga



Michael Jordan (kushoto) akimwadaha mpinzani wake

BAADA ya miaka 74 ya Ligi Kuu ya mpira wa Kikapu nchini Marekani, NBA, tumeshuhudia watu mashuhuri wengi na wenye viwango vya hali ya juu.

Pengine LeBron James au Michael Jordan? Bill Russell au Wilt Chamberlain? Stephen Curry au Kevin Durant?

Wote hawa ni nyota wenye kiwango kikubwa zaidi katika ligi ya NBA lakini wapo wenye mafanikio na historia bora zaidi kuliko wengine.

Wafuataao ni wachezaji mashuhuri zaidi katika ligi ya NBA na wenye vipaji vikubwa zaidi huku wakijenga historia kubwa katika ligi hiyo.

**5: Magic Johnson**

Johnson alibadilisha mchezo huo na kuingia kwenye ligi hiyo kama mzuiaji mrefu zaidi katika historia ya ligi akiwa na futi 6-9.

Bila Johnson na ushindani wake kwa enzi zile na Bird wa Celtics, NBA isingeweza kuwa hapa ilipo leo. Johnson aliyekuwa na kipaji kikubwa sambamba na mvuto aliipeleka Lakers ya "Showtime" hadi faainali tisa za NBA, na wakashinda mataji matano.

**4: Bill Rusell**

Mshindi mkubwa zaidi katika historia ya mpira wa vikapu, Russell alipata mataji 11 katika miaka 13 kwa kuwageuza Celtics kuwa magwiji wa ulinzi.

Ustadi wa ulinzi wa Russell na uthubutu ulimfanya kuwa msaada kamili kwa Wilt Chamberlain, na vile vile mmoja wa wachezaji kutoka enzi yake ambaye hangeonekana nje ya mahali katika vizazi vya baadaye.

Sifa hizo pia zilimsaidia kupata tuzo tano za MVP na chaguzi 11 za All-NBA.

**3: Kareem Abdul-Jabbar**

Hakuna mtu katika historia ya NBA anayeweza kufikia orodha ndefu ya mafanikio ya Abdul-Jabbar. Alishinda rekodi ya tuzo sita za MVP na alikuwa Nyota wa michezo mara 19.

Alishinda michuano sita huku ya kwanza na ya mwisho ikija tofauti kwa miaka 17 na alitajwa katika timu 15 za All-NBA, na alichaguliwa mara 10 kikosi cha kwanza cha mashindano ya NBA kwa msimu mmoja.

Nyota yake isiyozuilika ilimruhusu kufunga pointi nyingi zaidi kuliko mtu yeyote katika historia ya ligi.

**2: Lebron James**

MVP mara nne na bingwa mara tatu ni moja kati ya wachezaji tishio na wakutazamwa zaidi.

Alipokuwa na Lakers katika harakati za kuwinda taji kama mchezaji hodari akiwa na miaka 35 akicheza katika msimu wake wa 17 alipata Kizuizi cha kufukuzwa katika mchezo wa 7 wa fainali za mwaka 2016 na baadae kusaidia kukamilisha ushindi wa seti 3-1 dhidi ya timu ya Warriors ambayo ilishinda michezo kwa kuongoza wakiwa na alama 73.


**1: Michael Jordan**


Mchezaji bora wa wakati wote. Jordan aliiongoza Bulls kwenye michuano sita ya NBA, akishinda tuzo sita za Fainali za MVP na tuzo tano za MVP za msimu wa kawaida huku akiwa maarufu duniani ndani na nje ya uwanja.

Uzuri wa Jordan kwenye ncha zote mbili za uwanja ulifafanua kizazi cha mpira wa vikapu na kuweka kiwango kipya kwa wachezaji wanaofuata nyayo zake. Mchezo wake ulivuka kiwango cha kawaida cha uchezaji kutokana na ubora wake.



Lebron James


Kareem Abdul-Jabbar


Magic Johnson

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Aprili 17 - 23, 2024 |

## Wanariadha Afrika wapata kashfa China

**BEIJING, China**



UCHUNGUZI unafanyika juu ya mashindano ya Beijing Nusu Marathon kufuatia uwepo wa viashiria kuwa wakimbiaji watatu kutoka Afrika ambao ni Robert Keter na Willy Mnangat kutoka Kenya pamoja na Dejene Hailu kutoka Ethiopia kupunguza mwendo kwa makusudi ili kuhakikisha mkimbiaji wa China, He Jie anakuwa mshindi.

Katika video iliyozua gumzo, wakimbiaji hao wanaonekana wakipunguza mwendo na kumwashiria Jie aongeze kasi apite mbele.

## Fredy kutoka mshahara laki 6 hadi mil. 12 Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA Ronnie Santos ambaye alisimamia dili la beki wa Klabu ya Yanga Gift Freddy amefichua kuwa, wakati anamtafuta mchezaji huyo huko alipokuwa alikuwa akilipwa laki sita pekee lakini kwasasa akiwa na Yanga analipwa zaidi ya million 12.



Santos amekaririwa na Mtandao wa EKsports akieleza kwamba, katika kipindi cha hivi karibuni Ligi Kuu ya Tanzania imekuwa na ubora mkubwa hasa baada ya klabu mbili za Simba na Yanga kuanza kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa.

Wakala huyo wa Kimataifa amesema jambo hilo limewavutia nyota wengi kuja kuitumikia Ligi hii ya NBC ambapo licha ya ubora wake kuongezeka pia maslahi kwa wachezaji wengi ni makubwa.

"Gift Fred akiwa anaitumikia SC Villa alikuwa analipwa kiwango sawa na Tsh. 600,000 kwa mwezi, nikamfanyia mpango wa kulipwa zaidi ya shilingi milioni kwa 12 kila mwezi ndani ya Young Africans na jambo hilo likafanikiwa," amedai Santos.



## Majaliwa mgeni rasmi Tamasha la Dk. Samia

**Na Mwandishi Wetu**

SASA rasmi imethibitishwa kuwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa ndiye atakuwa mgeni wa heshima Jumamosi hii pale kwenye Viwanja vya TTCL Kijitonyama katika Tamasha kubwa la kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kazi za kutukuka alizozifanya ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake.

Kwa mujibu wa waandaaji Tamasha hilo Kampuni ya Uhuru Media Gruop wanaoshirikiana na "Bi Mkubwa Tanzania", wamepasha kuwa, maandalizi ya Tamasha hilo la miaka mitatu ya kishindo ya Dk. Samia, yamekamilika ikiwemo Waziri Mkuu Majaliwa kuthibitisha kwamba atakuwepo kwenye Viwanja vya TTCL Kijitonyama.

Uhuru Media Group imesema kuwa, kupitia udhamini wa wadau mbalimbali wenye mapenzi mema na uongozi wa Dk. Samia, Tamasha litakuwa la kukata na shoka kutokana na maandalizi kamambe yaliyofanyika ambapo kundi la Tanzania One Theatre (TOT) litaongoza burudani za wasanii mbalimbali walioalikwa.

"Njooni tumpe maua yake Rais wetu kipenzi, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwani kazi zake zinaongea!" Imesema taarifa hiyo ya Uhuru Media Group.

# Uongozi Simba matatani



- Wazungukwa kila kona na 'wenye klabu yao'
- Safu mpya yaandaliwa, Magori, Barbra ndani

**Na Mwandishi Wetu**

HALI si shwari ndani ya Klabu ya Simba na habari zilizonaswa na Uelekeo ni kwamba, inasubiriwa mechi na watani zao Yanga ipite Jumamosi hii ili waanze mikakati ya kutimua kiongozi mmoja baada ya mwingine.

Kwa mujibu wa chanzo chetu cha uhakika kilichoshiriki kikao kilichofanyika Jumamosi iliyopita baina Mwekezaji wao, Mohamed 'Mo' Dewji na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo.

Chanzo chetu hicho kimedokeza kuwa, Mo alihoji mambo mengi ikiwemo mwenendo mbaya wa timu yao kwenye michuano ya kimataifa na ya ndani, usajili na matumizi ya fedha anazotoa hususani zile za usajili.

"Kumekuwa na uvumi kwamba Mo amejiweka pembeni na hajataoa fedha zozote za kusaidia timu kwa zaidi ya mwaka jambo ambalo si la kweli, hivyo aliwataka viongozi wamweleza habari hizo zinatoka wapi kwani ni kinyume na hali halisi hivyo kwa upande wake," kimebainisha chanzo chetu.

Imeelezwa kwenye kikao hicho kilichohudhuriwa hadi na viongozi wa zamani waliojiweka au kuwekwa pembeni na shughuli za klabu, maamuzi ya mwisho yaliyofikiwa ni baadhi ya viongozi kutakiwa kuwajibika wenyewe au kuwajibishwa kupitia Bodi ya Wakurugenzi ya klabu ama uitishwe Mkutano Mkuu Maalumu wa Klabu wakajieleze mbele ya wanachama.

Kuna viongozi watatu wa juu (majina yao tunayahifadhi kwa sasa) hao ndiyo wamekalia kaa la moto baada ya kubebeshwa zigo la lawama kwamba hao ndiyo chanzo cha migogoro yote ndani ya klabu hiyo kiasi cha kusababisha timu yao isifanye vizuri kwenye ligi kwa mwaka wa pili sasa.

"Kuna kiongozi mmoja wa juu huyu ndiye yuko matatani zaidi, amewatenga hadi 'maligendi' wa klabu hiyo na kibaya zaidi hao ndiyo waliomkaribisha ndani ya Simba, hivyo nao wamemzunguka kila kona na sioni atatumia mbinu gani ili aendelee kubaki kwenye nafasi yake," amefichua mtoa habari wetu.

Mtoa habari wetu ameongeza kuwa, wahafidhina hao wa uongozi huu wa sasa wa Simba wameenda mbali kiasi kwamba tayari wameshaandaa safu yao mpya ya uongozi na kumkabidhi majina Mwekezaji wao Mo Dewji.

Majina yanayotajwa kwenye safu hiyo ni pamoja na Crescentius Magori, Jerry Yambi, Barbra Gonzalez na wengine wachache.

Juhudi za gazeti hili kuwapata viongozi wa Simba kuzungumzia sakata hili lilikwama kutokana na kutopokea simu zao, lakini hata hivyo Mshauri wa Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Magori mwishoni mwa wiki iliyopita aliwataka mashabiki wa Wekundu hao wa Msimbazi kutulia katika kipindi hiki kigumu.

Pamoja na kuongelea masuala kadhaa, pia alisema kuwa, baada ya mazungumzo yake na Mwekezaji wao Mo alimhakikishia kwamba bado yupo Simba na hajawahi kuiacha klabu hiyo na hatarajii kuiacha huku akiahdi kuendelea kushirikiana na viongozi wa Bodi yao ya Wakurugenzi.